SUPA JACKPOT
TZS. 1,069,861,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mwalimu** aingia matatani tuhuma adhabu ya kikatili kwa mwanafunzi

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Zama mpya kiutawala, kila Mtanzania kulikishiwa 'Bima ya Afya kwa Wote'
Shughuli za binadamu zinavyoteketeza mapito ya wanyama, kuongeza migogoro
Yaipatia sekta afya madaktari 1,560
Waziri Ummy: Asimilia 86 wenye umri kuanzia miaka 18 wamechanjwa Uviko

Nipashe
Alhamisi Januari 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581202
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11



TUNDU LISSU

# Hofu ilinitesa

• **Umati** wajitokeza kumpokea, Dar yasimama kwa muda... *Endelea ukurasa 2*



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwapungia mkono wananchi na wafuasi wa chama hicho waliojitokeza kumpokea baada ya kuwasili jijini Dar es Salaam jana. Picha nyingine: Matukio mbalimbali ya mapokezi hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 'Mkeka' wa Rais Samia waanza kusafisha ma-DC

UKURASA 3

**NJE**


Basila Mwanukuzi



Festo Kiswaga


Jerry Murro


Gabriel Zakaria

**NDANI**


Goodluck Asaph Mlinga- Liwale


Grace Kingalame-Nyang'halwe


Jaffar Haniu-Rungwe


Shaka Hamdu Shaka- Kilosa

**MICHEZO** NABI: NGUVU ZOTE KUONGEZA MABAO UK.24
**KATUNI** UK.6

# Umati wajitokeza kumpokea Lissu Dar

**Na Maulid Mmbaga**

HAYAWI hayawi, yamekuwa baada ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kuingia nchini na kupokewa na wafuasi wa chama hicho huku Jeshi la Polisi likiimarisha ulinzi na usalama katika barabara alizopita.

Lissu alitua majira ya saa 7:00 mchana katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam, huku mamia ya wafuasi wa chama hicho wakiwa wamevalia sare na bendera wakiimba nyimbo za kumkaribisha nchini akitokea Ubelgiji alikokaa kwa zaidi ya miaka sita.

Aliondoka nchini mwaka 2017 kwenda Kenya kwenye matibabu na baadaye alihamishiwa nchini humo ambako aliendelea na matibabu hadi mwaka 2020 aliporudi kwa ajili ya kugombea urais na kufanya kampeni nchi nzima na siku chache baada ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu aliondoka akisindikizwa na Balozi wa Ujerumani kwa kile alichodai ni kutishiwa maisha.

Baada ya maridhiano baina ya CHADEMA na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, chama hicho kilitangaza kukubaliana na kuendelea na mazungumzo na kuruhusu mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa baada ya kuzuiwa kwa takribani miaka mitatu na Lissu kutangaza atarejea nchini baada ya kuhakikishiwa usalama wake.

Msafara wa Lissu jana uliianzia uwanjani humo huku akiwa kwenye gari la wazi huku akiwapungia wafuasi na wananchi waliokuwa wamejipanga barabarani na magari yakisimamishwa kupisha msafara huo katika Barabara ya Nyerere, akielekea uwanja wa Mwembe Yanga, Temeke.

Wafuasi hao walisikika wakiimba nyimbo za 'karibu kamanda'... 'karibu rais na tunataka katiba mpya'.

Msafara wake uliambatana na magari na mamia ya wafuasi wa chama hicho, wananchi na wanafunzi wakionekana kuacha shughuli zao na kujipanga barabarani wengine wakiwa juu ya kuta za uzio kumshuhudia akipita na kunyoosha vidole viwili juu ishara inayotumiwa na chama hicho.

Katika msafara huo baadhi ya wafuasi waliobeba mabango yenye maandishi yaliyosomeka (Karibu Tundu Lissu mtetezi wa pekee wa wanyonge uliyebakia hakuna uhafadhari wa maisha) na (Tunataka Katiba mpya), pia msafara huo ulitumia zaidi ya saa mbili kufika viwanja vya Mwembe Yanga.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, alivyopokewa jana.

**KULAZIMIKA KUISHI NJE KUGUMU**

Akihutubia mamia ya wananchi uwanjani humo, Lissu alisema miaka mitano aliyoiishi nje ya nchi haikuwa rahisi kwake kwa wanachama wenzake na chama kwa ujumla, na kwamba ilikuwa ni mateso kuishi mbali kwa kuhofia usalama wake.

Alisema kwa sasa anafuraha kurejea rasmi nyumbani baada ya kukaa mbali na familia yake kwa zaidi ya miaka mitano na amekuja kwa ajili ya kazi aliyoitaja kuwa ni ngumu ya kusemea matatizo ya wananchi na kudai Katiba mpya.

"Nilishauriana na viongozi baada ya kushuka uwanjani kuliko niende sehemu kupumzika ni vizuri nipite niwasalimie Watanzania kwenye mkutano wa hadhara, miaka ya nyuma walikuwa wanasema hakuna kulala, nilipotangaza kurudi nilisema nitashukuru kwa maandalizi yoyote nitakayofanyiwa na hakuna kulala mpaka kieleweke," alisema Lissu.

"Ni muhimu kukumbuka huu ni mwaka wetu wa 30 wa chama naomba nikupongeze mwenyekiti na viongozi wote wa chama ngazi zote na Watanzania na wale wote waliotuunga mkono, safari ya miaka 30 Tanzania kama nchi ya vyama vingi haikuwa rahisi ilipambwa kwa miba na mawe kuna damu imemwagika," alisema Lissu.

"Watu waliteseka, walifungwa, wengine wamepotea hadi leo hawaonekani, tumeumizwa sana wote, hii safari haijawa rahisi kama tumefika hapa ni lazima tujipongeze licha ya magumu tuliyopitia, leo ndio kwanza nimekanyaga nyumbani kwetu naomba mniamini kuishi nje ya nchi kwa kulazimishwa kwasababu unaogopa kudhuriwa ni kitu kigumu ajabu," alisema Lissu.

"Hii miaka takribani sita haikuwa rahisi hata kidogo kwangu binafsi, kwa familia yangu, ndugu zangu, chama na nchi yangu, kwasababu ni miaka mitano ya kulazimishwa kuondoka nyumbani kwenu kwasababu usipoondoka kunawatu wametumwa wakuue, niseme nimefurahi kurudi nyumbani kwangu na kwetu," alisema.

Lissu alisema tatizo la maisha magumu ni la kiutawala, kisiasa na kikatiba, huku akiwasisitiza wananchi kuwa njia ya kutafuta suluhu ya matatizo hayo ni kutafuta Katiba mpya na kwamba tatizo kubwa linaloleta hayo yote ni Katiba.

"Tulivyotoka uwanjani tumepita kote nimesikia maneno mengi ya kwenu, nimesikia bei ya maharage inakuwa sawa na bei ya nyama, nikasema kukaa mbali unapitwa na mengi kila mahala watu wanalalamika maisha magumu sembe, maharagwe havikamatiki tozo kila mahali wanaopokea mshahara makato wanayokatwa ni mengi," alisema.

**MBOWE**

Alisema mwaka 2006 walipoamua kuzindua upya chama walirekebisha sera na kuziboresha tena 2018/19 na kwamba wakati wanafanya hivyo walikuwa kwenye kipindi kigumu na hawakuzitangaza kwa umma na sasa kwasababu wako kwenye anga na zama mpya (utawala wa Samia) watazitangaza.

"Ni wakati sahihi kwa viongozi kuanzia ngazi ya msingi wa chama watapewa sera za chama ili wazifafanue kwa wananchi, ili wakifahamu chama chao kinasimamia nini, baada ya mkutano tutagawa vitabu vya sera kwa Spika wa Bunge la Wananchi, Katibu Mkuu wa Chama, Naibu Katibu Zanzibar na Bara.

Mbowe alisema sera ndizo zilizoza ilani ya uchaguzi wa CHADEMA ya mwaka 2020 na kwamba hazikubuniwa na zinalinda falsafa za chama hicho kwa utetezi wa uhuru wa watu, haki za watu, demokrasia ya watu na maendeleo ya watu.

**KATIBA MPYA**

"Tumelisisitiza miaka yote na tutaendelea kusisitiza uwepo wa CHADEMA ni watu ndio msingi wetu, sisi tunajivunia nguvu ya umma. Mageuzi ya siasa za nchi yanapaswa kuanzia Dar es Saalam kwa sababu ndio jiji lenye wawakilishi kutoka kila kata nchini, kuna kila kabila imani na watu zaidi ya watu milioni 7.6 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi,"alisema.

Alisema mageuzi katika nchi zote yanaongozwa na majiji huku akitoa mfano wa Nairobi, Kenya na Zambia na kwamba ongezeko la watu ni 560,000 kwa mwaka na wote wanatokea mikoani na kuna kata 102, mitaa 566 na kila eneo lililoandikisha watu 1,000 watakuwa 566,000 ambao watakuwa na nguvu ya pamoja.

Mbowe alisema mwaka huu kuna uchaguzi ndani ya chama na kuwataka wanaotaka kuwa viongozi wajitokeze kwa wingi kwa kuwa chama sio mali yake na ni cha kila mwananchi na kwamba wasikae mkao wa kupumzika halafu wanataka Katiba mpya.

"Tunataka vijana wa kuandikisha watu kila mtaa watu 1,000, tukiwapata hao ni sawa na kujaza uwanja wa Mkapa mara nane, wanatosha kabisa kusukuma suala la Katiba mpya,"alisema.

"Mtu asikwambie CHADEMA ni chama cha porojo kinafanya utafiti wa mambo ya kuumiza wananchi la kwanza kwenye sera yetu ni Katiba, mambo ya msisitizo kama haki za binadamu, uhuru, utawala wa sheria na utoaji haki, sera ya rushwa, muungano na dhana ya ugatuaji madaraka, uchumi wa soko na kuna maeneo 18 yenye uchambuzi wa kina,"alifafanua.

Aidha, alimpongeza Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, kwa kuwapo kwenye mkutano huo na kwamba anaamini watatenda haki.



Kamanda wa Chuo cha Intelijensia cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Brigedia Jenerali TA Ntahena (kushoto), Brigedia Jenerali Peter Bailey wa Jeshi la Marekani Kamandi ya Afrika (katikati) na Mwambata wa Kijeshi wa Jeshi la Marekani nchini Tanzania, Kanali Gerald Mathis, wakitiliana saini mpango kazi wa ushirikiano rasmi baina ya majeshi ya nchi hizi mbili katika kilele cha mkutano wa siku mbili wa ushirikiano wa kiusalama uliowashirikisha maofisa waandamizi kutoka Wizara ya Ulinzi ya Marekani na JWTZ, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkeka wa Rais Samia waanza na maDC

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa wakuu wa wilaya wapya 37, akiwahamisha vituo vya kazi 48 na wengine 55 wakibaki kwenye maeneo yao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, miongoni mwa wakuu wa wilaya wapya ni aliyekuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, anayekwenda Kilosa mkoani Morogoro.

Wengine ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Mohamed Haniu, aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Rungwe.

Pia Rais amemteua aliyekuwa Mbunge Jimbo la Ulanga, Goodluck Mlinga kuwa Mkuu wa Wilaya ya Liwale na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Handeni Vijijini, Mboni Mhita kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama.

Baadhi walioachwa kwenye uteuzi huo na wilaya zao kwenye mabano ni Jerry Muro (Ikungi), Gabriel Zakaria (Busega), Basila Mwanukuzi (Korogwe), Festo Kiswaga (Kahama) na Sara Msafiri (Kibaha).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo kati ya wakuu wa wilaya 140, wanawake ni 40 na wanaume 100.

**WAPYA**

Wakuu wa Wilaya wengine na wilaya zao kwenye mabano ni Felician Mtahengerwa (Arusha), Marko Ngu'mbi (Longido) na Emmanuela Mtatifikolo (Arumeru).

Wengine Gerald Mongella (Chemba), Kanali Boniphace Magembe (Geita), Leah Ulaya (Mbogwe), Deusdedith Katwale (Chato), Grace Kingalame (Nyang'halwe) na Dk. Linda Salekwa (Mufindi).

Wengine Dk. Abel Nyamahanga (Muleba), Japhet Maganga (Kyerwa), Erasto Sima (Bukoba), Julius Laiser (Karagwe), Dinah Mathamani (Uvinza), Dk. Christopher Timbuka (Siha), Amir Mkalipa (Hai) na Kasilda Mgeni (Same) "Chistopher Ngubiagai (Kilwa), Beno Malisa (Mbeya), Josephine Manase (Kyela), Rebeca Msemwa (Morogoro), Rachel Kasanda (Magu).

Wakuu wa wilaya wengine ni Hassan Bomboko (Ukerewe), Victoria Mwanziva (Ludewa), Kanali Joseph Kolombo (Kibiti), Zephania Sumaye (Mafia), Lazaro Komba (Kalambo) na Dk. Jane Nyamsenda (Sumbawanga).

Wengine ni Wilman Ndile (Songea), Farida Mgomi (Ileje), Solomon Itunda (Songwe), Zakaria Mwansasu (Uyui) na Naitapwaki Tukai (Nzega).

**WALIOHAMISHWA**

Waliohamishwa vituo vya kazi ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda kwenda Monduli na Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, kwenda Ilala.

Halima Bulembo aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza amepelekwa Kigamboni, Hashim Komba aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea amekwenda Ubungo.

Wengine ni Mwanahamisi Mukunda aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi kwenda Temeke, Saadi Mtambule aliyekuwa Mkuu wa Wilaya Mufindi amehamishiwa Kinondoni.

Sophia Kizigo aliyekuwa Mkuu wa Wilaya Mkalama amehamishiwa Mpwapwa, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, amepelekwa Bahi, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Veronica Kessy, alipelekwa Iringa.

Wengine ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Nzega, ACP Advera Bulimba, amepelekwa Biharamulo, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga amepelekwa Mlele.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali amehamishiwa Kigoma, wa Uyui, Kisare Makori amepelekwa Moshi, Iringa, Mohamed Moyo, amekwenda Nachingwea.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kherry James amepelekwa Mbulu, wa Rungwe, Dk. Vicent Anney, amekwenda Bunda huku wa Ukerewe, Kanali Denis Mwila akipelekwa Mbarali.

Wengine walioguswa ni Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Sebastian Waryuba amehamishiwa Malinyi, wa Mtwara, Danstan Kyobya amekwenda Kilombero.

Wa Namtumbo, Dk. Julius Ningu, amehamishiwa Ulanga, Liwale, Judith Nguli anakwenda Mvomero, Uvinza, Hanafi Msabaha, amepelekwa Mtwara.

Wengine ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Luter Kanoni, amepelekwa Masasi, wa Kaliua, Matiko Chacha amekwenda Misungwi na wa Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija amekwenda Kwimba.

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta amepelekwa Wanging'ombe, wa Kigamboni, Fatma Nyangasa amepelekwa Kisarawe na wa Kisarawe, Nick John amehamishiwa Kibaha huku wa Mvomero, Halima Okash akienda Bagamoyo.

Wengine ni Mkuu wa Wilaya Mlele, Filberto Sanga, amehamishiwa Nyasa, wa Ulanga, Ngollo Malenya amepelekwa Namtumbo na wa Songwe, Simon Simalenga akihamishiwa Bariadi

**WANAOENDELEA NA VITUO**

Waliobaki katika vituo vyao kwenye mabano ni Dadi Kolimba (Karatu), Raymond Mangwala (Ngorongoro), Dk. Khamis Mkanachi (Kondoa), Remedius Emmanuel (Kongwa), Jabir Shekimweri (Dodoma) na Gift Msuya (Chamwino).

Wengine ni Said Nkumba (Bukombe), Peres Magiri (Kilolo), Kanali Wilson Christian Sakullo (Misenyi), Kanali Mathias Kahabi (Ngara), Jamila Kimaro (Mpanda), Onesmo Buswelu (Tanganyika) na Kanali Michael Ngayalina (Buhigwe).

"Kanali Evance Mallasa (Kakonko), Kanali Aggrey Magwaza (Kibondo), Kanali Issac Mwakisu (Kasulu), Kanali Hamis Maiga (Rombo), Abdallah Mwaipaya (Mwanga), Shaibu Ndemanga (Lindi) na Hassan Ngoma (Ruangwa).

"Janeth Mayanja (Hanang), Lazaro Twange (Babati), Mbaraka Alhaji Batenga (Kiteto), Dk. Suleiman Serera (Simanjiro), Dk. Halfan Haule (Musoma), Mwl. Moses Kaegele (Butiama), Dk. Vincent Mashinji (Serengeti), Juma Chikoka (Rorya).

"Lt. Kanali Michael Mtenjele (Tarime), Mayeka Mayeka (Chunya), Jabir Makame (Gairo), Lt. Kanali Patrick Sawala (Tandahimba), Mwangi Kundya (Newala), Mariam Chaurembo (Nanyumbu), Amina Makilagi (Nyamagana), Hassan Massala (Ilemela), Senyi Ngaga (Sengerema) na Juma Sweda (Makete)."

Wengine Kissa Kasongwa (Njombe), Khadija Ali (Mkuranga), Meja Edward Gowele (Rufiji), Peter Lijualikali (Nkasi), Julius Mtatiro (Tunduru), Aziza Mangosango (Mbinga), Joseph Mkude (Kishapu), Aswege Kaminyonge (Maswa), Faiza Salim (Itilima), Fauzia Ngatumbura (Meatu) na Paskasi Murangili (Singida).

"Fakii Lulandala (Momba), Sauda Mtondoo (Igunga), Abel Busalama (Kilindi), Hashim Mgandilwa (Tanga), Kalist Bukhay (Lushoto), Kanali Maulid Surumbu (Mkinga)," ilisema.

## M/Mkuu aliyempiga mwanafunzi viboko nyayoni asimamishwa kazi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Kakanja, wilayani Kyerwa mkoani Kagera, Issaya Emmanuel, amesimamishwa kazi na kuvuliwa cheo kwa kumpa adhabu ya viboko miguuni huku akiwa amemkanyaga.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Kagera,

Albert Chalamila, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani humo, baada ya video iliyosambaa ikimwonyesha mwalimu huyo akimtandika mwanafunzi huku walimu wengine wakicheka.

Aidha, ameagiza kuchukuliwa hatua za haraka walimu wanne waliokuwa wanacheka wakati mkuu huyo akimwadhibu mwanafunzi huyo, huku akizitaka kamati za shule kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Kwa mujibu wa Chalamila, tukio hilo lilitokea Januari 10, mwaka huu, ambalo ni kinyume na waraka wa elimu namba 24 wa mwaka 2002, unaoelekeza utaratibu wa adhabu shuleni.

Chalamila alisema ufuatiliaji wa awali umeonyesha kuwa mwalimu huyo aliwaadhibu watoto hao kwa madai ya kutofanya mazoezi ya ziada (home work) waliyopewa wakati wakienda likizo.

Aliwataja wanafunzi walioonekana wakiadhibiwa ni Salmon Kakwezi (9) na Anold Kweyamba (10) wote wa darasa la nne.

Alisema kinacholeta shida ni namna adhabu hiyo ilivyotolewa kwa watoto hao, bila kujali kuwa inaweza kuathiri afya zao.

"Waraka huo unasema adhabu itazingatia ukubwa wa kosa, umri, jinsi na afya ya mtoto, na isizidi viboko vinne kwa wakati mmoja, kwa hiyo kosa la kwanza ni kupiga viboko zaidi ya vinne na kwa kuwa aliyetoa adhabu hiyo ni mwalimu mkuu alistahili," alisema na kuongeza:

"Kosa lake lingine hakuandika kwenye kitabu maalumu baada ya adhabu hiyo, pia upigaji wake wa kuwakanyaga wanafunzi kwa mguu wake huku akiwapiga kwenye nyayo, unahatarisha afya za wanafunzi."

Chalamila alimwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Toba Nguvila, kumchukulia hatua za kisheria Mratibu wa Elimu Kata ya Kakanja, kwa kushindwa kuchukua hatua za haraka za tukio hilo.

Pia aliagiza awachukulie hatua za kinidhamu walimu wanne, wanaoonekana kwenye kipande hicho cha video wakiwa wanacheka, wakati mwalimu mkuu akitoa adhabu hiyo.

Walimu hao ni Godson Rwabwisho, Beatrice Osward, James Josiah na Delphina Leonce.

"Walimu ambao wanapaswa kuwa walezi na washauri wa mwalimu mkuu, wakaonekana hawakufanya jukumu lao wakawa wanacheka na kukiuka jukumu hilo, tuombe radhi Watanzania kwa jambo lililotokea ambalo linaumiza na kusisimua, hasa ilivyoonekana mtoto alivyopigwa na kuanza kuchechemea," alisema Chalamila.

Alihakikishia wananchi kamati za kiuchunguzi zinaendelea kulifanyia kazi suala hilo, ili kupata vigezo vinavyostahili na mwalimu huyo aweze kufikishwa mahakamani mara moja.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka (katikati), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi wa Kituo cha Mazingira cha New Delhi India (CSE), Jagdeep Gupter baada ya kutiliana saini makubaliano ya kuangalia ubora wa maji Ziwa Victoria, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mary Maganga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Zumaridi ahukumiwa jela mwezi mmoja

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MCHUNGAJI Diana Bundala maarufu 'mfalme Zumaridi,' amehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja jela na wenzake wanne baada ya kukutwa na hatia katika makosa mawili kati ya matatu.

Katika hukumu hiyo washtakiwa wengine wanne wameachiwa huru baada ya kutokutwa na hatia.

Zumaridi atatumikia kifungo cha mwezi mmoja baada ya kuondolewa miezi 11 aliyokaa mahabusu.

Wanne waliachiwa kwa masharti ya kutokujihusisha na kosa la jinai ndani ya mwaka mmoja na kutakiwa kuripoti polisi kila baada ya miezi mitatu kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa wa Mwanza, Monica Ndyekobola, baada ya kusikilizwa kwa ushahidi wa pande zote mbili, Jamhuri na utetezi na kubaini kuwa walikuwa wakikabiliwa na makosa matatu ya kushambulia na kumdhuru ofisa wa polisi, kuwazuia maofisa wa polisi kutekeleza majukumu yao na kumzuia ofisa wa serikali kutekeleza agizo la mahakama.

Aidha, katika makosa mawili hukumu ilionesha kuwa washtakiwa wanne kati ya wanane walikiri kuagizwa na Zumaridi kushiriki kuwazuia maofisa wa polisi na ofisa ustawi wa jamii.

Hakimu Mkazi Mfawidhi Monica alisema, watuhumiwa wote tisa hawakukutwa na hatia katika kosa namba moja la kumshambulia ofisa wa polisi na kudhuru mwili kutokana na ofisa huyo ambaye alikuwa shahidi namba mbili kushindwa kueleza vyema katika ushahidi wake.

Kabla ya hukumu hiyo pande zote mbili zilipata nafasi ya kujieleza kuhusu maamuzi yatakayotolewa na mahakama hiyo na Hakimu Ndyekobora alisema kosa hilo hukumu yake inaweza kuwa kifungo chake ni miaka mitano kwa kuzingatia mwongozo wa utoaji wa adhabu wa mahakama katika kigezo cha sheria ya kosa husika.

Akitoa hoja za upande wa Jamhuri Wakili wa Serikali, Ghati Matayo, alisema washtakiwa wote wanatakiwa kupatiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

Wakili wa upande wa utetezi wakiongozwa na wakili Erick Muta, waliomba mahakama hiyo kupunguza adhabu hiyo kutokana na watuhumiwa hao kukaa mahabusu kwa miezi 11 na kuwafanya wapate funzo na kujutia makosa yao.

Aidha alisema kwa upande wa mshtakiwa namba moja anategemewa na mama yake mzazi ambaye ni mgonjwa, watoto wake na wengine 34 wanategemea msaada wake wa chakula, mavazi pamoja na kusomeshwa.

Pia alisema anategemewa na wanawake wajane na kwamba hukumu yake ikiwa kali watu hao watakosa msaada.

Zumaridi anakabiliwa na kesi ya kusafirisha binadamu ambayo haina dhamana inayotarajiwa kuanza kusikilizwa ushahidi wake Januari 27 na kumfanya abaki mahabusu katika kipindi chote tangu mwishoni mwa mwezi Februari mwaka jana alipokamatwa pamoja na wafuasi wake.

Mara ya kwanza Machi 3, 2022 wafuasi 92 pamoja na Zumaridi walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza na kusomewa mashtaka yao.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani Machi 3, mwaka jana ikiwa ni takribani siku saba tangu walipokamatwa nyumbani kwa mchungaji huyo eneo la mtaa wa Buguku, Kata ya Buhongwa jijini Mwanza.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
26.01.2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumapili tarehe 29-01-2023 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero** kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili: **T 515 BKC / T 387 DHQ T 416 DFE / T 273 DUH T 695 BNQ / T 150 CHN T 694 BNQ / T 146 CHN**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 23.00**
   **Upana - mita 4.30**
   **Kimo - mita 5.20**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi**, gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217243702



TAARIFA KWA UMMA



MELIANA WATSON MWAIGAGA



FELIX AJUNA JOSEPH

**Q & R REAL ESTATE INVESTMENT na JARIQ INVESTMENT** tunapenda kuutarifu umma kuwa watajwa hapo juu **MELIANA WATSON MWAIGAGA** na **FELIX AJUNA JOSEPH** ambao picha zao zimebandikwa hapo juu SIYO wafanyakazi wetu tena kuanzia tarehe 20/01/2023.

Hivyo kamapuni zote mbili HAZITOHUSIKA na miamala, mikataba au biashara yoyote watakayofanya.

117243802


## NEMC yapendekeza utumike usafiri wa umma kulinda mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limependekeza kuimarishwa kwa usafiri wa umma kama ilivyo kwa mabasi ya mwendo wa haraka na kupunguza matumizi ya magari binafsi ikiwa ni mkakati wa kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa.

Limesema kuna umuhimu serikali ikaimarisha miundombinu ya usafiri ili wananchi wengi waweze kutembea kwa miguu na baiskeli badala ya kutumia magari.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka, wakati wa kongamano la kimataifa linalojadili usafiri wa nchi kavu na uchafuzi wa hali ya hewa kwa nchi 10 za Afrika.

Nchi zinazowakilishwa kwenye mkutano huo wa siku tatu ni pamoja na Kenya Zambia, Zimbabwe, Ethiopia, Uganda Rwanda, Msumbiji, Ghana, Nigeria na Mauritius.

"Tumekutana hapa kubadilishana uzoefu kuhusu kila mmoja anachofanya ili kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa kwenye miji yetu kwasababu uchafuzi wa hewa unaathiri sana afya za wakazi wa hiyo miji, kwa hiyo jitihada kama hizi lazima zifanyike," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema kuna visababishi vingi vya uchafuzi wa hali ya hewa kama viwanda kwa kiasi kikubwa, lakini magari hasa yale chakavu ni chanzo kikubwa cha uchafuzi wa hali ya hewa.

Alisema maendeleo yamesababisha ongezeko kubwa la magari maeneo ya mijini kiasi cha kusababisha hata kukosekana maegesho ya kutosha hivyo kuongeza tatizo la hali ya hewa.

"Magari mengi yanayoagizwa ni yale yaliyotumika miaka mingi kwa hiyo kutokana na kuwa chakavu yanatoa hewa chafu na kuchafua hali ya hewa na mazingira kwa ujumla. Kwa hiyo mkakati hapa ni kuhamasisha matumizi ya usafiri wa umma kupunguza haya magari," alisema.

Alisema ili kufanikisha mpango wa kupunguza matumizi ya magari kuna umuhimu wa kujenga barabara zitakazokuwa na maeneo mazuri ya watembea kwa miguu na waendesha baiskeli kama ilivyo kwenye nchi zilizoendelea.

"Watu wa mipango kama TANROADS waweke mikakati kuhakikisha barabara zinakuwa rafiki kwa watembea kwa miguu na waendesha baiskeli. Kwa hiyo tuanze kuboresha sheria na kanuni zetu kuanzia sasa," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Mazingira, New Delhi India (CSE), Jagdeep Gupte, alisema mkutano huo ni wa 10 kwa nchi za Afrika kukutana na kujadiliana kuhusu namna ya kuondokana na uchafuzi wa mazingira na usafiri wa nchi kavu.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa FreedomPath Tanzania Limited, Deusdedit Kabunduguru, akipiga mnada mali za kampuni ya uzalishaji wa majani ya chai ya Rift Valley Tea Solution. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mali za kampuni zapigwa mnada kulipa michango wanachama NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

MALI za kampuni ya uzalishaji wa majani ya chai, Rift Valley Tea Solution Limited, zimepigwa mnada ili kulipa michango ya wanachama wa NSSF baada ya kushindwa kuwasilisha michango hiyo zaidi ya Sh. milioni 226.

Kampuni ya udalali wa Mahakama, FreedomPath Tanzania Limited ilipiga mnada mali hizo kwa idhini ya Mahakama ya Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam katika shauri la madai namba 93/2022.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa FreedomPath Tanzania Limited, Deusdedit Kabunduguru, alisema katika shauri hilo mdai ni Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) dhidi ya kampuni hiyo ambaye alishindwa kuwasilisha fedha za michango ya wafanyakazi wake NSSF na Mfuko kuamua kufungua kesi mahakamani ili mwajiri huyo alipe michango ya wafanyakazi wake ambayo ipo kwa mujibu wa sheria.

"Leo (juzi) tulikuwa tunashughuli ya kuendesha mnada wa hadhara kwa maelekezo ya Mahakama ya Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, ambapo ilikuwa ni kesi namba 93/2022 mdai akiwa ni Bodi ya NSSF dhidi ya kampuni ya Rift Valley Tea Solution Limited ambapo mdaiwa huyo alishindwa kuwasilisha fedha za michango ya wafanyakazi wake na NSSF iliamua kufungua kesi mahakamani ili aweze kulipa michango ya wafanyakazi," alisema.

Kabunduguru alisema wanashukuru wameweza kupata mshindi wa mnada huo na kuwa NSSF inaweza kupata fedha za michango ya wanachama na hatimaye wafanyakazi wa kampuni hiyo wataweza kupata haki zao.

"Nitoe rai kwa waajiri kuhakikisha wanawasilisha michango ya wafanyakazi wao kwa wakati ili kuepuka madhila kama haya," alisema.

Kabunduguru alisema NSSF ilikuwa inaidai kampuni hiyo michango ya zaidi ya Sh. milioni 226 na wafanyakazi walikuwa hawajaingiziwa michango kwa zaidi ya miaka mitatu.

Naye Geofrey Sikira, Kaimu Meneja Mwendesha Mashauri wa NSSF, alisema Mfuko kwa amri ya Mahakama imeuza mali ya mwajiri huyo kwa mujibu wa sheria.

"Tunachofanya ni utaratibu wa kawaida kabisa, kwani mwajiri anaposhindwa kulipa michango ya wafanyakazi wake tunampeleka mahakamani na tukishinda kesi hatua za kimahakama zinafuata ambazo ni kuuza mali za mwajiri kwa kutumia dalali wa mahakama," alisema Sikira.

Alifafanua kuwa, mwajiri anapaswa kuwasilisha michango ya wanachama wake kila mwezi na akikaa kwa miezi sita bila kuwasilisha anakuwa ni mdaiwa ni kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

"Natoa wito kwa waajiri wa sekta binafsi kutii sheria kwa kulipa michango ya wafanyakazi wao kwa wakati ili waweze kuendelea na shughuli mbalimbali za uzalishaji kwenye kampuni zao," alisema.

Ramadhani Juma, aliyeshinda mnada huo, alisema ameunua mtambo huo kwa Sh. milioni 167 ambao utaenda kuongeza thamani ya zao la chai kwa kuchakata chai na kuiweka katika soko la kimataifa.

# Wawili mbaroni tuhuma kuvua samaki kwa baruti kilo 980

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji jijini Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa wawili wanaodaiwa kukutwa na samaki kilo 980 wanaosadikika kuvuliwa kwa baruti.

Kamanda wa kikosi hicho, Moshi Sokoro, alisema jana kuwa samaki hao wamekamatwa wakiwa kwenye boti ya uvuvi yenye namba za usajili Z 103585 MV Maedra.

Alisema wamekamatwa Januari 12, maeneo ya Soko la Samaki Feri baada ya operesheni kufanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Kamanda Sokoro aliwashukuru wananchi wanaochukia uhalifu na kuwaomba waendelee kutoa taarifa ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema Jeshi la Polisi litachukua hatua kwa yeyote atakayehusika na uvuvi haramu pamoja na makosa mengine ya jinai.

# Wadau wataka viwango stempu za ETS vipungue

**Na Frank Monyo**

WAZALISHAJI wa bidhaa za tumbaku, vileo na vinywaji nchini wameiangukia serikali wakiiomba ipunguze gharama za Stempu za Ushuru za Kielektroniki (ETS) zinazotumika kwenye bidhaa wanazozalisha.

Ombi hilo lilitolewa na wazalishaji hao baada ya kukutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika kikao kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.

Kikao hicho kiliandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), wazalishaji, wakiwamo Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Serengeti Breweries Limited (SBL), Kampuni ya Sigara ya Umma (TCC Plc), Coca-Cola Kwanza na SBC (T) Ltd (Pepsi).

Mkurugenzi Mkuu wa Coca-Cola Kwanza, Sulai Unguu, alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kampuni yake imelipa zaidi ya Sh. bilioni 13 kununua stempu za ETS wakati ushuru unaolipwa ni Sh. bilioni 34.2.

Alisema gharama ya huduma zikiwa ni sawa na asilimia 38 ya ushuru wa bidhaa inayolipwa kwa serikali.

Kadhalika alisema, katika kipindi cha miaka minne juhudi zao za kutaka gharama hizo kushushwa zimegonga mwamba huku maombi waliyoomba katika idara mbalimbali za serikali kutokuwa na matokeo chanya.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema kwa kipindi cha miaka minne iliyopita kampuni yake ilinunua stempu za ushuru zenye thamani ya karibu Sh. bilioni 27 sawa na asilimia nane ya malipo yote ya ushuru.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL Plc, Jose Moran, alisema ETS sio kodi bali ni mfumo wa kuweka alama za fedha ambao uliundwa kwa madhumuni ya kuhesabu uzalishaji kwa wakati halisi na vilevile kurasimisha sekta kwa uwanja sawa.

Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Hamis Mwinjuma ni mwenyekiti wa kikao hicho, aliwaahidi wazalishaji hao kuwa suala hilo litawasilishwa bungeni ili kutafutiwa ufumbuzi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapendekezo ya NEMC muhimu kufanyiwa kazi

**UCHAFUZI** wa hali ya hewa unaosababishwa na moshi wa viwandani na magari mabovu, limekuwa tatizo kubwa duniani na Tanzania ikiwamo.

Tatizo hili linaathiri afya za watu na kusababisha magonjwa yakiwamo ya saratani na serikali kuingia gharama kubwa ya kuagiza dawa.

Katika kongamano la mazingira linalofanyika jijini Dar es Salaam na kukutanisha nchi 10 kutokana Afrika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limependekeza kuimarishwa kwa usafiri wa umma nchini Tanzania kama ilivyo kwa mabasi ya mwendo wa haraka na kupunguza matumizi ya magari binafsi ikiwa ni mkakati wa kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa.

Baraza hilo limesema kuna umuhimu serikali ikaimarisha miundombinu ya usafiri ili wananchi wengi waweze kutembea kwa miguu na baiskeli badala ya kutumia magari.

Tunaungana na NEMC katika mapendekezo hayo, kwa sababu katika baadhi ya nchi zilizoendelea wameweka kipaumbele kwenye matumizi ya baiskeli kama njia ya usafiri badala ya magari ili kupunguza hewa ya ukaa ambayo inachafua mazingira.

Njia zilizopendekezwa ikiwamo watu kutembea kwa miguu husaidia pia kuwaweka katika afya imara na kuwaepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Kuendesha baiskeli na kutembea kwa miguu ni mazoezi mazuri yanayomfanya mtu kuimarika kiafya na kujiepusha kila mara kumwona daktari kwa sababu ya kusumbuliwa na magonjwa.

Nchi zinazowakilishwa kwenye kongamano hilo la siku tatu ni pamoja na Kenya, Zambia, Zimbabwe, Ethiopia, Uganda, Rwanda, Msumbiji, Ghana, Nigeria na Mauritius.

"Tumekutana hapa kubadilishana uzoefu kuhusu kila mmoja anachofanya ili kupunguza uchafuzi wa hali ya hewa kwenye miji yetu kwasababu uchafuzi wa hewa unaathiri sana afya za wakazi wa hiyo miji, kwa hiyo jitihada kama hizi lazima zifanyike," alisema Dk. Samuel Gwamaka, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC.

Kuna visababishi vingi vya uchafuzi wa hali ya hewa kama viwanda kwa kiasi kikubwa, lakini magari hasa yale chakavu ni chanzo kikubwa cha uchafuzi wa hali ya hewa.

Nchi nyingi zinazoendelea kimaendeleo kunasababisha ongezeko kubwa la magari maeneo ya mijini hivyo kuongeza tatizo la uchafuzi wa hali ya hewa.

Kwa mujibu wa NEMC, magari mengi yanayoagizwa ni yale yaliyotumika miaka mingi na kuwa chakavu matokeo yake yanatoa hewa chafu na kuchafua hali ya hewa na mazingira kwa ujumla.


Baraza hilo limeona haja ya kuhamasisha matumizi ya usafiri wa umma kupunguza wingi wa magari barabarani.

Pia umuhimu wa kujenga barabara zitakazokuwa na maeneo mazuri ya watembea kwa miguu na waendesha baiskeli kama ilivyo kwenye nchi zilizoendelea.

Takwimu zinaonesha namna gani uchafuzi wa hali ya hewa umekuwa chimbuko kubwa la maradhi mengi Afrika na duniani na jitihada zisipochukuliwa afya za watu wengi duniani zitakuwa shakani.

Tanzania uchafuzi wa hali ya hewa ni tatizo ingawa hewa safi kulinganisha na nchi zingine za Afrika, lakini bado kuna mengi ya kufanya kufikia viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO), kuhusu uchafuzi wa hali ya hewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Siku ya Elimu itukumbushe nafasi ya mazingira kwa vitendo shuleni

Na Jenifer Gilla

**MNAMO** Januari 24 ya kila mwaka, dunia inaadhimisha Siku ya Elimu, mwaka huu kaulimbiu ni 'Wekeza kwa Watu Elimu iwe Kipaumbele'. Hapo ina maana kuwa, elimu ndio msingi ya kuleta maendeleo na mabadiliko katika nyanja zote.

Akitoa salamu katika maadhimisho Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Pro. Adolf Mkenda, anasema serikali inatoa elimu kwa kuzingatia usawa, ujumuishi, ubora na uhalisia na kuhakikisha hakuna kundi litakaloachwa nyuma.

Aidha, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), lilitoa ujumbe mkuu kuwa elimu ipewe kipaumbele katika kuharakisha kuyafikia malengo ya maendeleo endelevu na kushughulikia mdororo wa kiuchumi, kuongezeka ukosefu wa usawa na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Wakati mikakati ya kuleta mageuzi katika elimu ikiendelea kwa kuyapa kipaumbele masomo kwa vitendo ili kuandaa vijana wanaokidhi ajira na masoko ya kimataifa, hakuna budi kuangalia namna ya kupenyeza somo la mabadiliko ya tabianchi linalotishia kurudisha nyuma juhudi za kuyafikia mendeleo endelevu.

Wote ni mashuhuda wa namna janga hilo linavyoathiri sekta za maendeleo nchini hasa zile muhimu za vyakula, kilimo, afya na viwanda ambavyo kwa kiasi kikubwa vinabeba dhana ya ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja, jamii na taifa kwa ujumla.

Baadhi ya maeneo yaliyokuwa yanazalisha nafaka kwa wingi kama vile sehemu za mkoa Morogoro, pia wilaya ya Handeni mkpani Tanga, uzalishaji wake mazao umepungua, kutokana na ukame uliosababishwa na mvua kutonyesha kwa kiwango kilichozoeleka na kusababisha bei za vyakula hivyo kupanda.

Kwa mujibu wa Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, mabadiliko ya tabianchi yanasababisha mvua kutotabirika, kunyesha kwa kiwango cha chini au cha juu tofauti na kinachohitajika hali inayoathiri shughuli za kilimo.

Aidha, anasema kuwa tabia ya nchi pia inasababisha kuwapo kwa joto kali ambapo kwa sasa limefikia nyuzi joto 1.09 ambalo husababisha joto kuwa kali na kuathiri ukuaji wa mazao, ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji.

Ili kukabiliana na janga hilo jamii inapaswa kutunza mazingira ikiwamo kuhifadhi miti iliyoko na kuendelea kupanda miti kuzalisha hewa ya oksijeni ya kutosha itayosafisha hewa ya kaboni ambayo husababisha joto kuwa kali, hali ya hewa isiyotabirika.

Suala la kutunza miti linaonekana kuwa kitendawili nchini pamoja na juhudi zinazoendelea kufanywa na serikali pamoja na wadau wa mazingira, ikiwamo kutoa elimu na kuhamasisha jamii kupanda miti, sababu kubwa ikiwa ni kuwa miti ndio chanzo kikuu cha nishati ya kupikia ya bei nafuu, pia jamii haijalichukulia jambo hili kwa uzito stahiki.

Hapo basi tunahitaji kupenyeza elimu ya upandaji miti shuleni, ili kuwafundisha watoto katika umri mdogo kuhusu umuhimu wa kutunza miti na kuwajengea utamaduni wa kupanda miti, ili wawe na mazoea hayo, huku wakiepuka kutumia nguvu kubwa ya usahawishi wanapokuwa wakubwa.

Ili kulifanikisha hilo, serikali ina nafasi yake katika kushirikiana na asasi za kiraia, pamoja na walimu kwa kuwapa ruzuku za kuendesha miradi shuleni, kwa kuwa bila msaada huo, jambo hilo haliwezi kufanikiwa.

Zipo asasi za mazingira zinazofanya kazi kubwa ya kuelimisha watoto kuhusu kupanda miti na kuwapelekea miti wanafunzi shuleni, kama vile Shirika la Utu na Mazingira(HUDEFO), ambazo zimekuwa zikililia serikali na wadau wengine kuwaunga mkono kwa kuwa inafika mahali wanashindwa kutokana na uhaba wa fedha.

Pia wazazi tuna nafasi yetu kuiunga mkono serikali katika kampeni ya kupanda miti hata majumbani, ili kuwafundisha watoto wetu umuhimu wa kuwa na mito hiyo, kupata vivuli, hewa safi na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

HABARI KITAIFA

# Laini za simu milioni mbili zisizohakikiwa kuzimwa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imesema Februari 13, mwaka huu, laini za simu zaidi ya milioni 2.3 zitazimwa, kutokana na kutohakikiwa ili kukomesha vitendo vya utapeli mitandaoni.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema hayo juzi jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema mpaka Januari 19, mwaka huu, kuna laini za simu zinazotumika 60,739,790 na zilizohakikiwa ni 58,432,669, huku laini 2,307,121 sawa na asilimia 3.8 hazijahakikiwa.

"Kwa muda mrefu kumekuwa na utapeli mwingi unaoendelea wa kutumia simu na jambo hili linaongezeka sana kadri laini za simu zinavyoongezeka, sasa wizara kupitia mamlaka ya mawasiliano tulichukua hatua za usajili wa alama za vidole, tulianza Mei mosi, 2019 na kufungwa Desemba 2021."

"Kila laini iliyolengwa wakati ule kusajiliwa kwa kweli ilisajiliwa na tukaanzisha kampeni ya pamoja ya kuhakiki ambayo inaendelea hadi sasa na tulikubaliana mwisho ni Januari 31, 2023 kama namba hujahakiki hiyo namba itazimwa," alisema.

Alisema kuna laini nyingi mtaani ambazo watu wametumia vitambulisho vya watu wengine kusajili laini na zinazozimwa ni zile ambazo zimesajiliwa kwa uongo.

"Tumelenga kuwaondoa matapeli kwenye mfumo. Tumesema tuongeze siku nyingine 14 kuanzia Januari 31 hadi Februari 13, saa 10 jioni, siku moja kabla ya wapendanao tunataka anga la mtandao liwe salama ili kusiwe na matapeli wa kusema 'ile nauli nitumie huku'," alisema.



Mtuhumiwa wa kosa la mauaji ya mke wake Naomi Marijani, Khamis Luwonga (mwenye shati jeupe), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza baada ya kesi yake kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam juzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Aliyeshtakiwa kumuua mke kwa kumchoma amwangukia Samia

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani kwa kumchoma moto kwa kutumia magunia ya mkaa, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwashughulikia watumishi wa ofisi ya waendesha mashtaka.

Amedai watumishi hao wameshindwa kumjibu barua zake alizowaandikia kuhusu kutomuua mkewe kwa kukusudia.

Aidha, alidai kuwa wakati akiwa kituo cha polisi alikiri kumuua mkewe bila kukusudia kwa kuwaeleza ukweli wote polisi namna tukio hilo lilivyotokea hadi anapoteza maisha (mkewe).

Luwonga alitoa ombi hilo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ramadhani Rugemalira wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo iliyoitwa kwa ajili ya kutajwa.

"Nakuomba hakimu unipe dakika mbili nizungumze kidogo, kuna jambo linanishangaza sana na ni la ajabu, kuna baadhi ya wafanyakazi wa upande wa mashtaka wanafanya mambo ya ajabu sana.

"Rais Samia Suluhu Hassan naomba ushughulikie watumishi hawa kwa sababu nimeshaandika barua ya kukiri kumuua mke wangu bila ya kukusudia, lakini hadi leo wananizungusha wana kazi ya kuondoa kesi na kuileta upya," alidai Luwonga.

Pia alidai ofisi hiyo sio nzuri kidogo kwa sababu kipindi cha Hayati Rais Dk. John Magufuli, aliandaa barua katika ofisi ya waendesha mashtaka, lakini hajajibiwa.

Baada ya madai hayo, Hakimu Rugemalira alimuuliza mshtakiwa wakati kesi hiyo ikiwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga, alikiri kosa hilo kama alivyodai.

Luwonga alidai hakuweza kukiri kwa sababu Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya mauaji.

Hakimu alimuuliza tena wakili wa mshtakiwa, Mohamed Majaliwa, ambaye alijibu hakuwahi kukiri.

Pia Luwonga alidai kuwa wakati aliposomewa maelezo ya kesi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shahidi, Oktoba 21, 2020, alikana kumuua mke wake kwa kukusudia.

"Unajua kesi za mauaji zipo za aina mbili kuua kwa kukusudia na kuua bila kukusudia, kwa hiyo wewe umeshtakiwa kwa kuua kwa kukusudia," alisema Hakimu Rugemalira.

Akijibu swali la Hakimu, Luwoga alisema: "Ni kweli hakimu, nimeshtakiwa hivyo, lakini mimi sikumuua mke wangu kwa kukusudia ndiyo maana niliandika barua. Serikali ilitoa fedha nyingi kuleta mashahidi, lakini badala ya kesi kuendelea wao wakaiondoa wakanisomea upya shtaka na kudai upelelezi haujakamilika."

Hata hivyo, Hakimu Rugemalira alimtaka mshtakiwa awe na subira kwa sababu wakili wake, Majaliwa amepeleka maombi Mahakama Kuu kwa hiyo wasubiri majibu na kuahirisha kesi hiyo hadi Februari 7, 2023.

Awali, Wakili wa Serikali, Mosie Kaima alidai kuwa wapo kwenye hatua za kuwasilisha taarifa Mahakama Kuu, lakini Wakili Majaliwa alidai kuwa wamefungua maombi katika mahakama hiyo ili kuangalia uhalali wa kesi mpya iliyofunguliwa.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimuua Naomi Marijani.

Hamis anadaiwa kumuua mke wake Naomi kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na kuchukua majivu ya marehemu na kwenda kuyafukia shambani kwake.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa 31.12.2022 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30.09.2022 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 54,749 | 56,072 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 60,422 | 33,436 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 103,603 | 105,901 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 69,156 | 78,791 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 271 | 499 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 98,960 | 129,413 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 841,590 | 821,878 |
| | 12 | Mali Nyingine | 39,970 | 43,904 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 21,207 | 21,075 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,289,929** | **1,290,968** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 862,393 | 834,456 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 124,778 | 147,846 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 2,206 | 6,238 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | (0) | (0) |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 24,428 | 20,855 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 2,641 | 2,723 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 28,084 | 25,644 |
| | 28 | Madeni | 129,401 | 134,672 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,173,931** | **1,172,434** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **115,998** | **118,534** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 31,372 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 71,781 | 71,792 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,152 | 5,677 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 9,694 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **115,998** | **118,534** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 151,019 | 108,694 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 72,800 | 70,393 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15,323 | 13,790 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1,736 | 1,761 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.99% | 9.18% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.43% | 8.36% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 87.44% | 85.76% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.24% | 63.66% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.95% | 81.89% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 0.50% | -2.57% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -0.08% | 0.52% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 36.323 | 36.106 | 139.994 | 135.181 |
| 2 Gharama za Riba | (12.635) | (11.502) | (48.198) | (40.509) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **23,688** | **24,605** | **91,797** | **94,672** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 104 | (362) | (500) | (519) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3.400) | (3.311) | (13.750) | (13.649) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **7.553** | **9.432** | **34.400** | **34.503** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1.960 | 1.636 | 5.925 | 5.561 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 3.793 | 5.403 | 17.568 | 18.732 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 1.800 | 2.392 | 10.906 | 10.210 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(27,395)** | **(25,578)** | **(100,707)** | **(95,127)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 12.798 | 11.572 | 49.094 | 45.988 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 3.562 | 1.261 | 9.060 | 4.615 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 11.035 | 12.746 | 42.553 | 44.524 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **549** | **4,786** | **11,240** | **19,879** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 3.074 | 1.950 | 8.088 | 8.640 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2.525)** | **2.836** | **3.152** | **11.238** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(2.525)** | **2.836** | **3.152** | **11.238** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1.086 | 1.091 | 1.086 | 1,091 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (80) | 101 | 100 | 400 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 48 | 47 | 48 | 47 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.20% | 0.24% | 0.25% | 1.01% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -2.14% | 2.46% | 2.70% | 10.17% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 62.44% | 56.17% | 57.75% | 56.06% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.27% | 2.58% | 9.00% | 10.68% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 549 | 3.479 | 11.240 | 19.879 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 6.371 | 6.878 | 25.698 | 25.816 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (19.712) | (51.265) | (122.990) | (100.786) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4.868 | (25.921) | 79.055 | 116.199 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (181) | 3.004 | 3.173 | (7.627) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 3.933 | 2.468 | (1.064) | (3.087) |
| - Kodi Iliyolipwa | (3.074) | (1.521) | (8.088) | (8.640) |
| - Menginevo (bainisha) | (3) | 5.261 | (1.528) | (41.365) |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(7,249)** | **(57,617)** | **(14,504)** | **388** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (728) | (279) | (2.921) | (8.549) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa | - | - | - | (8.549) |
| Menginevo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(728)** | **(279)** | **(2,921)** | **(17,098)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (1,652) | (2,366) | (6,456) | (6,791) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(1,652)*** | ***(2,366)*** | ***(6,456)*** | ***(6,791)*** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (9,629) | (60,263) | (23,881) | (23,501) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **97,424** | **157,687** | 111,676 | **135,177** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 87,795 | 97,424 | 87,795 | 111,676 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 3,152 | **3,152** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | **3,667** | - | (3,667) | - | - | - | **(0)** |
| Mengineyo | **(367)** | - | - | - | | - | **(367)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **71,780** | **(0)** | **0** | **12,846** | **115,998** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 9,167 | - | - | - | **9,167** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (253) | - | - | - | **(253)** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA, 2022

Benki ililipa faini ya shilingi 19,455,000.00 kutokana na upungufu wa fedha zilizopelekwa Benki kuu(Bot counter shortage), kushindwa kuomba kibali cha ukarabati wa majengo, na kuchelewesha taarifa ya mapato ya kodi TRA (TRA Returns)

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI (Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **Imesainiwa** | **23.01.2023** |
| **REGINA E. SEMAKAFU (Mkuu wa Fedha)** | **Imesainiwa** | **23.01.2023** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE (Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | **Imesainiwa** | **23.01.2023** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | **Imesainiwa** | **23.01.2023** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI** Mjumbe wa Bodi | **Imesainiwa** | **23.01.2023** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

2172444802

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES 2022

*All charges are VAT exclusive.

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | MINIMUM OPERATING BALANCE | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | 7,000.00 | 5.00 | 50,000.00 | 100.00 |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | FREE | N/A | 50,000.00 | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | 1,800.00 | 0.86 | 20,000.00 | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | 1,800.00 | N/A | 0 | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000.00 | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | FREE | FREE | 50,000.00 | N/A |
| Platinum Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 5,000 | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | FREE | N/A | 20,000 | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 0 | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000 | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | FREE | N/A | 30,000 | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | 1,800.00 | N/A | 10,000 | N/A |
| Wadu Account | 20,000.00 | N/A | FREE | FREE | 20,000 | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | 700.00 | N/A | 1,500.00 | N/A |

## CASH SERVICES

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Cash deposit | | FREE |
| | Withdrawal below 400,000 | 1,800.00 |
| | Withdrawal 400,001 - 800,000 | 3,000.00 |
| | Withdrawal from 800,001 - 1,200,000 | 4,400.00 |
| | Withdrawal from 1,200,001 - 10,000,000 | 5,000.00 |
| | Withdrawal from 10,000,001 - 50,000,000 | 6,000.00 |
| | Withdrawal from 50,000,001 -100,000,000 | 14,000.00 |
| Cash withdrawal TZS | Withdrawal from above 100,000,000 | 0.12% max 170,000 |
| | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| **BANK STATEMENT** | **TZS** | **USD** |
| Balance enquiry over the counter | 1000.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| **CHEQUE SERVICE** | **TZS** | **USD** |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00 per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

## AGENT BANKING SERVICE

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 3,000, 000.00 | 10,000.00 |
| Balance Enquiry | | 100.00 |
| Mini Bank Statement | | 200.00 |

## POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Registration | | FREE |
| | 500 -10,000.00 | 850.00 |
| | 10,000.01 - 50,000.00 | 1,200.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 1,500.00 |
| | 100,000.01 - 250,000.00 | 2,800.00 |
| | 250,000.01 - 500,000.00 | 4,600.00 |
| | 500,000.01 - 750,000.00 | 7,500.00 |
| Transfer Bank to MNO | 750,000.01 - 1,000,000.00 | 10,000.00 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

| LOANS | CATEGORY | RATE |
|---|---|---|
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 20,000.00 |
| | Loan Application fee | TZS 20,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 20,000.00 Maximum TZS 150,000.00 |
| | MIC loan Application fee | TZS 150,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 150,000.00 |
| | Loan Application fee for Business Loans | TZS 20 0,000.00 |
| Charges on Business Loan | Loan Administration fee - Business and Personal loans | 2% of the Approved Amount |

## DORMANT ACCOUNT

| | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

## POPOTE ATM SERVICE

| ACTIVITY | BAND[TZS] | New Charge (TZS) |
|---|---|---|
| 1. ATM Cash Withdraw | 1,000 – 99,000 | 1,500 |
| | 100,000 – 400,000 | 1,700 |
| 2. Interbank transfer on ATM | 1 – 99,999 | 1,300 |
| | 100,000 - 199,999 | 1,700 |
| | 200,000 - 299,999 | 1,700 |
| | 300,000 - 399,999 | 1,700 |
| | 400,000 - 499,999 | 2,500 |
| | 500,000 - 599,999 | 3,000 |
| | 600,000 - 699,999 | 3,500 |
| | 700,000 - 999,999 | 4,000 |
| | 1,000,000 - 1,999,999 | 5,000 |
| | 2,000,000 - 2,999,999 | 6,000 |
| | 3,000,000 - 3,999,999 | 7,000 |
| | 4,000,000 - 4,000,000 | 8,000 |
| 3. Intra-Bank Transfer on ATM | Any Amount | 1,000 |
| 4. Balance Inquiry | NA | 400 |
| 5. Mini Statement | NA | 400 |
| 6. Popote ATM card issuance /Replacement | N/A | 15,000 |
| 7. PIN Re-issue | N/A | 1,000 |
| 8. Collection of ATM card at non-domicileBranch | N/A | 6,500 |
| 9. Uncollected and Destroyed ATM Card | N/A | |
| 10. Card Maintainance | N/A | 5,000 |
| 11. Failed Transaction Due to insufficient fund | | 900 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

## GUARANTEE

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

## POPOTE VISA CARD

| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote VISA issuance/Replacement | 20,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,350.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 5,500.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |

## TCB BANK POPOTE VISA CARD

Accepted at all Visa outlets Point of Sales (POS) and Online platforms worldwide





*Apply for your Popote card at your nearest TCB Branch/ Online!*

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together
VISA

217244802

Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683 Namba bila Malipo: 0800110160



# TANESCO yaonya 'vishoka' mradi wa REA vijijini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), wilayani Kahama mkoani Shinyanga limetangaza kiama kwa watumishi wasiokuwa waadilifu wanaoshirikiana na mafundi 'vishoka' kuwauzia wananchi nguzo za umeme za mradi wa REA.

Pia limewataka viongozi wa serikali za vijiji, jeshi la jadi (Sungusungu) kwa kushirikiana na ofisi za watendaji wa kata kuwakamata 'vishoka' hao pindi wanapowabaini na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Kahama, Tumaini Chonya, alitoa kauli hiyo jana wakati wa mkutano wa hadhara katika Kata ya Sabasabini Halmashauri ya Ushetu baada ya kupokea malalamiko ya wananchi juu ya kuuziwa nguzo za umeme na baadhi ya mafundi ambao wanasema ni watumishi wa shirika hilo.

Alisema kwa sasa kata hiyo haina mkandarasi anayetekeleza mradi wa REA mpaka hapo baadaye serikali itakapoleta kampuni nyingne na kwamba vishoka wanaopita vijijini kuuza nguzo za umeme wakamatwe kwani kitendo bicho kinalihujumu shirika.

Alisema vitendo hivyo havivezi kuvumilika na kuwataka wananchi kuwafichukua kwa kutoa taarifa.

"Mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi wa REA katika kata hii mkataba wake uliisha na sasa tuko katika hatua za kumpata mwingine ili aendelee kusambaza huduma, anayeuza nguzo hapa ni tapeli na anatakiwa kuwajibishwa kwa sababu, REA hawauzi nguzo kwa wananchi," alisema Chonya.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Sabasabini, Michael Mihambo, alisema nyumbani kwake aliwekewa nguzo ya umeme kupitia mradi wa REA, lakini baada ya mwezi mmoja iliondolewa na kwenda kuuzwa kwa matajiri wa kijiji wenye viwanda kitendo ambacho hakikumfurahisha na sasa amepoteza matumani ya kupata huduma.

Alisema vijijini wazee wananyanyasika kupata huduma hususani wasiokuwa na fedha hawawezi kupata umeme kama serikali ilivyoelekeza.

Diwani wa kata hiyo, Emmanuel Makashi aliomba shirika hivyo kuangalia namna ya kupata mkandarasi mwingine atakayeongeza kasi ya usambazaji wa huduma ili iweze kuwanufaisha wakazi wa vijiji sita vya kata hiyo na kuondokana na adha ya kutapeliwa fedha zao na vishoka wanaopita vijijini kuuza nguzo.

Alisema baadhi ya wananchi wenye fedha wameunganishiwa huduma na vishoka wanaojinasibu ni watumishi wa shirika hilo bila idhini ya TANESCO.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema wamepokea Sh.bilioni mbili ambazo zitasambaza huduma ya umeme katika kata 20, vijiji 112 pamoja na vitongozi 564 na hivi karibuni atapatikana mkandarasi mwingine na kuanza kusambaza huduma hivyo.



Mkuu wa Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, Dk. Khalfan Haule (mwenye kofia), akishiriki kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya Kijiji cha Muhoji, Kata ya Bugwema jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wazingira nyumba kutaka kuwaona wachawi

**Elizabert Seleman,** SENGEREMA

JESHI la Polisi wilayani Sengerema mkoani Mwanza limetumia mabomu ya machozi kutawanya mamia ya wananchi waliokuwa wameizingira nyumba iliyokuwa ikisadikiwa ndani kuna watu wanaodaiwa ni wachawi.

Watu hao wanaodaiwa kuwa ni wachawi walishindwa kuondoka katika nyumba ya mkazi mmoja wa Kitongoji cha Kanyamwaza, Kata ya Mwabaruhi wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Wakizungumzia tukio hilo baadhi ya wananchi walisema kuwa jambo hilo limezua taharuki katika eneo hilo na kuitaka jamii kuachana na imani za kushirikisha.

Wananchi hao walisema hakuna sababu ya kuendekeza vitendo vya ushirikina na badala yake wanatakiwa kufanya kazi ili kujiletea maendeleo yao.

Aidha, wananchi hao walisema masuala ya kwenda kufanya vitendo vya ushirikina kwa mtu yameshapitwa na wakati badala yake wanapaswa kumrudia Mungu.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kanyamwaza, Laulian Philipo, alikiri kuwapo kwa kundi la wananchi kuizingira nyumba ya mkazi huyo anayefahamika kwa jina la Chrizandi Caroli.

Alisema baada ya Jeshi la Polisi kuingia ndani ya nyumba hiyo hawakuwaona watu hao wanaosadikiwa kuwa ni wachawi jambo lililoacha maswali mengi kwa jamii.

# H'shauri, mkandarasi SGR waanza mazungumzo kuhusu ushuru

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Shinyanga iko kwenye mazungumzo na mkandarasi anayejenga Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Mwanza hadi Isaka, China Civil Engineering Constraction Corporation (CCECC), ili kuanza kulipa ushuru wa madini ya ujenzi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Manispaa ya Shinyanga kilichohusu kupitisha mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha (2023/2024) Sh. bilioni 36.8.

Hatua hiyo imekuja baada ya Diwani wa Mwanza, Juma Nkwambi, kuhoji juu ya kuibua vyanzo vipya vya mapato.

Kwenye hoja yake Nkwabi alihoji kwa nini chanzo hicho cha madini ujenzi hakikusanywi na kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri ili kufikia malengo waliojiwekea ya kukusanya Sh. bilioni sita katika mwaka huo wa fedha 2023/2024.

Alisema manispaa hiyo kwa sasa ipo kwenye mazungumzo na mkandarasi huyo ili kukubaliana kuanza kulipa ushuru wa madini ujenzi ambayo wanatumia kwenye ujenzi wa reli hiyo ambayo ni mchanga na moramu.

"Chanzo hiki kipya cha madini ujenzi tutakifuatilia ili kuanza kutoza ushuru pia huyu mkandarasi ambaye anajenga reli ya SGR, ambayo inapita hadi Shinyanga amekuwa akichimba madini ujenzi, lakini halipi kitu, sasa hivi tupo kwenye mazungumzo naye ili waanze kulipa mapato," alisema Tesha.

Aliwaahidi madiwani hao kwamba halmashauri hiyo itaendelea kuibua vyanzo vipya vya mapato, huku akiomba ushirikiano kwa madiwani wanapokuwa wakiona chanzo kipya cha mapato, washirikishe menejimenti ili wakifuatilie.

Awali akichangia mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha (2023/2024), Nkwambi alisema ili kufikia malengo waliojiwekea ya kukusanya mapato ya ndani Shilingi bilioni sita wanapaswa kuibua vyanzo vipya vya mapato yakiwamo madini ujenzi kuanza kutoza ushuru.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, aliwataka watumishi ambao wanakusanya mapato kuboresha kanzi data zao ili wawe wanapata taarifa za mara kwa mara kwa wafanyabiashara ambao wameshalipa mapato. Kadhalika, aliwaonya pia watumishi hao wanapokuwa wakikusanya mapato kwa wafanyabiashara wasitumie nguvu wala lugha chafu, bali wawapatie elimu juu ya faida ya kulipa kodi, kwamba fedha hizo zinawarudia wenyewe kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha, Mchumi wa Manispaa ya Shinyanga, Mensaria Mrema, akisoma taarifa ya mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha (2023/2024) alisema halmashauri inatarajia kukusanya Sh.bilioni 36.8.





**Zama mpya kiutawala, kila Mtanzania kufikishiwa 'Bima ya Afya kwa Wote'**






Shughuli za binadamu zinavyoteketeza mapito ya wanyama, kuongeza migogoro





# Waziri Ummy: Asimilia 86 wenye umri kuanzia miaka 18 wamechanjwa Uviko

**Na Yasmine Protace**

MARA zote inaelezwa katika teknolojia ya afya, chanjo ni nyenzo muhimu inayolinda, kukinga na kusaidia kuokoa maisha ya mtu na zipo za aina nyingi, kila moja na lengo lake, kwa ujumla ni kumsaidia awe salama kiafya.

Kuna ushuhuda hata abiria mwenye safari kwenda nchi nyingine anakingwa kwa chanjo, asipatwe na maambukizi ya aina fulani ya magonjwa. Huduma hiyo hufanyika hata katika ngazi ya viwanja vya ndege vya kimataifa.

Uwapo wa maradhi ya Covid-19 mwaka 2020, haukuiacha Tanzania salama kwa namna nyingi, kama ilivyo mataifa mbalimbali, hata kusababisha watu kupoteza maisha kutokana na ugonjwa huo.

Katika kupambana, mikakati ya kitaifa kukabili virusi vya Uviko - 19 imekuwa ni utoaji elimu kwa jamii kupata chanjo yake.

Serikali nchini imekuwa katika harakati za chanjo dhidi ya maradhi hayo, kazi kuu iliyoanza mwaka jana hata kufanyika taratibu maalum za kuwafikia wananchi waliko.

Kumekuwapo vituo vya afya vya kiserikali na binafsi vikihusika kutoa chanjo, ili kuifanikisha jamii ijikinge dhidi ya balaa hilo la kiafya.

Serikali imekuwa ikiwahamasisha watu kuchanja kwa hiari Uviko -19, kampeni iliyozinduliwa na Rais kuchanja, pia watendaji waandamizi kiserikali, lengo ni kuwawezesha wasipate maambukizi mapya ya virusi hivyo, huku ikitoa ripoti ya kazi yake.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Afya kuhusu utekelezaji bajeti ya wizara yake kuanzia Julai 2022 hadi Desemba. **PICHA: YASMINE PROTACE**

### NENO LA WAZIRI

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba 2022, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya, wamefanikisha chanjo dhidi ya Uviko -19, kufikia asilimia 86 ya Watanzania wenye umri kuanzia miaka 18.

Kwenye taarifa ya utekelezaji Bajeti ya Wizara ya Afya kwa kipindi kati ya Julai na Desemba mwaka jana kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii jijini Dodoma, anasema ni hatua ikilinganishwa asilimia 24.7 kufikia Juni, 2022, umma ukiendelea kupata dozi kamili ya chanjo hiyo.

Hapo anaainisha takwimu za dozi husika, akisema hadi kufikia tarehe 31 ya mwezi uliopita, kuna jumla ya dozi 46,848,520 zilizopokewa na kati yao dozi 41,581,670 (asilimia 88.75) zilikuwa zimesambazwa nchi nzima.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, kiasi cha chanjo kilichosalia kwenye bohari ya kutunzia chanjo ni 5,266,850 ambazo zote ni aina ya J.J.

Anaongeza kuwa, Wizara ya Afya hivi karibuni itazindua 'booster' dozi ya UVIKO-19, ili wananchi waweze kuongeza kinga zaidi dhidi ya ugonjwa huo na kusema kuwa ni hiari kwa mtu yeyote kwenda kupata chanjo hiyo.

Waziri anasema huduma hizo zinaendelea kutolewa kwa watoto wa chini ya umri mwaka mmoja, kwa chanjo iitwayo 'Penta3' inayotumika kipimo kikuu ilifikia asilimia 107, ikilinganishwa na mwaka 2021 iliyofikiwa kwa asilimia 9.6.

Waziri Ummy anasema, Wizara ya Afya imeshafanikisha vyema kampeni ya utoaji wa chanjo ya polio ya matone (OPV3) katika mizunguko yote minne kwa asilimia 103, ikilinganishwa na asilimia 79 mwaka 2021.

Pia anataja sindano ni kwa asilimia 107 ikilinganishwa na asilimia 95 kwa mwaka 2021; surua rubella, dozi ya kwanza ni asilimia 109, ikilinganishwa na asilimia 92 kwa mwaka 202; surua rubella dozi ya pili, ni asilimia 96, ikilinganishwa na asilimia 76 mwaka 2021.

"Kwenye utoaji wa chanjo ya kukinga saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana, dozi ya kwanza tulifanikisha utoaji wa chanjo hiyo kwa asilimia 83 ikilinganisha asilimia78 kwa mwaka 2021.

"Chanjo ya kujikingana saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana dozi ya pili (HPV2) asilimia 62 ukilinganisha na asilimia 61 kwa mwaka 2021," anafafanua.

Anasema, wizara imeendelea kuboresha huduma za afya mipakani na kuhakikisha kuwa magonjwa ambukizi yaliyoko katika nchi jirani hayaingii nchini.

"Tumefanya kazi kubwa ya usimamizi wa masuala ya afya mipakani kuhakikisha ugonjwa wa ebola hauingii nchini na habari njema tumesikia hivi karibuni nchi ya Uganda, imetangaza kumaliza mlipuko wa ugonjwa wa ebola. Kwa hiyo na sisi tunaamini tupo salama," anasema.

### KAMATI BUNGE

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Afya, Stanslaus Nyongo, anaipongeza Wizara ya Afya na taasisi zake, kuendelea kusimamia vyema Sera ya Afya na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya.

Nyongo anaishauri Wizara ya Afya, kushirikiana vyema na Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa, kuhakikisha kuna usimamizi imara katika utoaji huduma bora za afya kwa wananchi.

AFYA

# Zama mpya kiutawala, kila Mtanzania kufikishiwa 'Bima ya Afya kwa Wote'

**Na Waandishi Wetu**

MWONGOZO wa utendaji nchini katika mfumo unaotawala, hoja kuu za kiserikali huanza na kupata ridhaa ya kisiasa chini ya mtawala, Chama Cha Mapindizi (CCM).

Ndicho kilichofanyika mnamo Juni 24 mwaka jana, Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM chini ya Mwenyekiti Rais Samia Suluhu Hassan, ikaridhia mapendekezo ya kuwa na Bima ya Afya kwa Wote nchini, kwamba yatawasaidia wananchi uhakika wa huduma za matibabu.

Hatua hiyo ya kiserikali, inayosimamiwa na Rais Samia, kuifikisha kwenye chama kupata baraka kabla ya kurejeshwa kwenye mfumo wa serikali kwa hatua zaidi, ikiwamo kuwatambua wasiokuwa na uwezo nao wanufaike.

Ni hali inayofanana na hatua kama hiyo hivi karibuni, Rais Samia alipowahakikisha waombaji wote wa ufadhili mikopo ya elimu ya juu wenye sifa, wananufaika.

Akizungumza mnamo Septemba mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, kwenye Jubilee ya Miaka 50 ya Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), akatamka:

"Niwaombe sana tutakapopitisha sheria hii Watanzania tukajiunge na mifuko ya bima. Nawapa uhakika tunajua udhaifu uliopo kwenye mifuko yetu ya bima."

"Mfuko huu utahakikisha mtu anapata matibabu yote anayopaswa kupata. Huu ni kama upatu ambao Watanzania wote tunakwenda kucheza, upatu huo na kati yetu anayepatwa na shida, upatu huo unamsaidia," anafafanua.

Kimsingi, Bima ya Afya ni mkataba ambao mtu ama analipiwa au kulipia, kupata huduma maalum za kimatibabu ambazo ziko chini ya kivuli cha bima maalum.

### WAZIRI UMMY/ BOSI NHIF

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema bima ya afya ni utekelezaji wa Ilani ya CCM kupitia uchaguzi mkuu uliopita, inayozitaja mifuko tajwa NHIF na CHF, ili ikilenga kufikia lengo la serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote.

Akiwasilisha mapendekezo ya kuimarisha Mfumo wa Bima ya Afya nchini kwa wajumbe wa NEC, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga, anaeleza itasaidia kuwapo utaratibu unaomwezesha mwananchi kupata huduma tofauti nchini, kwa baadhi ya bima ya afya.

Faida nyingine anaitaja, ni kuwapa wananchi wote mafao yanayofanana, hata wakaondoa matabaka ya kijamii. Miezi minne baadaye, akitoa taarifa kwa umma kuhusu tija inayowekezwa, Waziri Ummy akasema:

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, zilikuwa wastani wa 6871 2021 na hadi mwaka jana zilikuwa 10,380, ikiendana na watumishi 100,000, kutoka 86,000 wa mwaka 2015/2016.

"Hii itasaidia kwa Watanzania wote kupata huduma bora za afya bila kikwazo cha fedha, pia serikali itahakikisha dawa zinapatikana kwa wakati na zinazokidhi mahitaji ya wagonjwa," anasema Waziri Ummy.



Rais Samia Suluhu Hassan, alipoutangazia umma ujio wa Bima ya Afya kwa Wote, katika kikao cha Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), mjini Dodoma, Septemba mwaka jana. **PICHA: MAKTABA.**

> **"Hii itasaidia kwa Watanzania wote kupata huduma bora za afya bila kikwazo cha fedha, pia serikali itahakikisha dawa zinapatikana kwa wakati na zinazokidhi mahitaji ya wagonjwa.**

### KINACHOENDELEA SASA

Hivi karibuni Wizara ya Afya iliwasilisha bungeni Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya. Pia, serikali imeunda kamati maalumu kuratibu utoaji elimu kwa umma kuhusu bima ya afya kwa wote.

Ni mpango chini ya Wizara ya Afya, ukilenga kumfikia kila Mtanzania, mahsusi mama na watoto, kwa kurejea mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO); takwimu zikionyesha ni kundi linaloathirika na kupanda kwa gharama za matibabu kifamilia.

Wataalamu wa kiafya duniani wanafafanua kuwa ni kundi linalotumia zaidi huduma za afya, kutokana na sababu za kibaiolojia na kimaumbile.

Aidha, wakati taifa linatajwa imefanikiwa kuboresha Ustawi wa Afya za Watanzania, pia inatimiza malengo endelevu ya dunia kufikia afya na ustawi mwema na kuendeleza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia inatajwa suala la afya limebaki kuwa mtambuka kwa kila Idara, kitengo na taasisi kutenga pesa za kutumikia bajeti ya kutoa elimu ya afya kwa jamii.

Rai iliyoko ni ya wote wahusika kuaandaa mipango ya afya, hasa makatibu wa afya kuanzia ngazi ya wizara, mkoa na halmashauri, ambao kimsingi ndio waratibu na wasimamizi wa mipango na bajeti katika Idara ya Afya.

Ni aina ya mikakati sasa imewekwa katika Mipango na Bajeti, ili kutekelezwa katika mwaka wa mpya wa fedha 2023/2024.

### MWELEKEO ULIKOFIKIA

Hivi karibuni Wizara ya Afya ilipeleka Bungeni muswada wa Bima ya Afya kwa Wote nchini na kamati maalumu imeundwa kuratibu utoaji elimu kwa umma.

Pia hatua iliyoko sasa, kwa mujibu wa Waziri Ummy, ni kwamba bima hiyo iko njiani kuwasilishwa bungeni kwa mara nyingine kwenye kikao kijacho, huku ikifafanuliwa umuhimu wake.

Chini ya uratibu wa Wizara ya Afya, kunatarajiwa kuhakikishwa upatikanaji wa bima ya afya kwa wananchi wote nchini, kukilenga mahsusi kundi la kinamama na watoto, ambayo takwimu zinaonyesha ni kundi linaloathirika zaidi na kupanda gharama za matibabu kifamilia na kijamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya duniani, hilo ni kundi linalotumia zaidi huduma za afya, kutokana na sababu za kibailojia na maumbile, hivyo ujio wa mpango huo unatajwa kuwa mkombozi wa kundi hilo, familia na wananchi wote nchini kwa ujumla.

Inashauriwa, wote wanaohusika na uaandaaji wa mipango ya afya hasa makatibu wa afya kuanzia ngazi ya wizara, mkoa na halmashauri, ambao kimsingi ndio waratibu na wasimamizi wa mipango na bajeti katika katika idara za afya, inajulikana kwa sasa kama wawajibike ipasavyo.

### ORODHA YA FAIDA

Mchakato huo uliopitishwa chini ya uongozi wa Rais Samia, faida zilizoko zinajumuisha; kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya afya muda wowote anapoihitaji, bila ya kutegemea kipato chake wakati huo.

Inaelezwa kupitia mpango huo, kila mtu atakuwa na kadi ya bima kumwezesha kupata huduma za afya kwa mwaka mzima, pasipohitaji la kulipia tena huduma hizo.

Ni hatua inayotajwa kwenda sambamba na kuondoa kuwapo ama kaya au familia, zinazotumia gharama kubwa zaidi ya kipato chao katika matibabu ya wanakaya wake.

Ni hali inayofanya familia kufilisika kutokana na matatizo ya afya. Pia upatikanaji bima ya afya kwa wote, inatajwa itawapunguza wananchi kuchelewa kwenda vituo vya afya kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya afya, ikikwepa gharama kubwa.

Hadi sasa, umma huo unatajwa kwa sasa watatumia kadi zao na si fedha tena kama hapo awali. Ni hali inayopunguza vifo, ulemavu na madhara ya kaifya yatokanayo na kuchelewa uchunguzi wa afya, wakipata matibabu kwa wakati.

Inatajwa ni mpango utakaoisaidia serikali kuwa na uhakika wa kuhudumia afya wananchi wake, pia kuhakikisha wananchi wake wanakuwa na afya njema, hata wakashiriki katika ujenzi wa taifa lao.

Pia unatajwa unaotoa funzo katika utekelezaji mradi husika au mingine inayaofanana na mradi tajwa wa bima ya afya kwa wote nchini na hata mazingira yanayofanana, mtazamo ukielekea kwenye lengo, mwaka 2030.

***• Waandishi wa makala hii; Elifuraha Msese (+255 758242923) Katibu wa Afya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, pia ni mtaalamu wa Masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya; pia Pankras Luoga (+255 757645746), ni Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya, katika- Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.***

AFYA

# Shughuli za binadamu zinavyoteketeza mapito ya wanyama, kuongeza migogoro

**Na Salome Kitomari**

MIGOGORO baina ya wanyamapori na binadamu inazidi kuongezeka, hali inayosababisha kutoelewana kwa watu na wanyama wanapoteza maisha, pia kukosekana amani baina yao.

Kwa sasa, karibu kila eneo la hifadhi kuna migogoro ya wanyama watokao hifadhini kupita mapito yao au shoroba, ambako binadamu nako wameanzisha shughuli zao kama majengo na mashamba, hivyo wanyama wanapopita na kula wanaonekana waharibifu.

Pia ukame hivi sasa unawafanya wanyama wakose maji na malisho, wanatoka hifadhini kufuata mahitaji muhimu kwenye maeneo ya kibinadamu, ndipo migogoro baina yao inatokea, kunakuwapo viumbe wanaohama, wanajeruhiwa au kuuawa.

Shoroba ni njia zilizopo kisheria, wanazopita wanyamapori, kutoka eneo moja lililohifadhiwa kwenda jingine kutafuta mahitaji muhimu kama malisho, maji na madini muhimu kwenye maeneo ya mtawanyiko, ili kukamilisha ikolojia inayowahusu.

Penye mtawanyiko, ndiko wanyama wanapata madini maalum ya miili yao wakijiandaa kuzaa katika kukamilisha mzunguko wa kiikolojia. Njia zao ni penye shoroba zilizoanzishwa wanyama, waendelee kuwa salama na kuondoa migogoro.



Ilivyo hali halisi, wanyama wakipita kwenye shoroba zao ndani ya hifadhi za wanyama nchini.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

### WANAHABARI WAHUSISHWA

Katika kuzilinda shoroba hizo, kuwanusuru wanyama wasitawanyike nje ya njia zao, Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya RTI kupitia mradi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) Tuhifadhi Maliasili, wamepata mafunzo za kuwasaidia waibue habari za kulinda shoroba, waweze ama kupunguza au kumaliza migogoro baina ya pande hizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, anasema ni mradi unaolenga kuwajengea uwezo wanahabari kuibua habari za uhifadhi wa wanyamapori, hasa kwenye shoroba saba nchini na kuwaelimisha Watanzania umuhimu wa sekta binafsi kushiriki.

John Noronha, ni Meneja Ufuatiliaji na Tathmini USAID Tuhifadhi Maliasili, katika mada yake ya 'Mwingilio wa Maisha Baina ya Wanyamapori na Binadamu kuwa kipaumbele cha Taifa kwa Maendeleo Endelevu na Uhifadhi Wanyamapori Tanzania', anasema takwimu za mwaka 2012 hadi 2019 zinaonyesha migogoro inazidi kuongezeka kwenye ukanda huo.

> **Katika kila kikao bungeni, kumekuwapo sauti za kulalamikia uharibifu wa mazao, watu kuuawa, pia kujeruhiwa na wanyamapori, wakiitaka serikali kuchukua hatua stahiki.**

Anatumia takwimu za kipindi hicho, kwamba zaidi ya watu 1,069 waliuawa na wanyama, 642 walijeruhiwa na wengine kupatwa na ulemavu wa kudumu.

Pia anataja ekari 41,404 za mazao yaliyoharibiwa, mifugo 792 iliuawa na kujeruhiwa, vyote hivyo vikiigharimu nchi shilingi bilioni 4,67 (Sh. 4,670,555,300).

Anataja sababu kubwa ya migogoro hiyo, ni ongezeko la watu kulikosukumwa na hitaji la ziada la ardhi na rasilimali, kutokuwapo ujumuishi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na shoroba na maeneo ya mtawanyiko kutowekwa kwenye Gazeti la Serikali.

Nyingine anataja, kuongezeka matumizi ya maji kunakofanywa na binadamu kwa shughuli za nyumbani na kiuchumi, mpango wa matumizi bora ya ardhi usiokidhi mabadiliko ya tabianchi.

Noronha anasema, kuongezeka shughuli za kijamii ni muhimu kuweka uhimilivu wa kibinadamu, hasa kwa wanaotegemea chanzo kimoja cha mapato ambalo ni eneo lililohifadhiwa, inayoweza kuathirika uvumilivu wa wanyama.

"Kwa Tanzania kuna dhana iliyojengeka kuwa serikali inawajibika kwa wanyamapori. Kadri imani ya kijamii katika taasisi inavyoonekana kuwajibika kwa wanyamapori, ndivyo uwezekano mkubwa zaidi wa watu wanapaswa kutambua hatari ndogo zinazohusiana na wanyamapori," anafafanua.

Pia, anapendekeza mbinu za kukabili migogoro hiyo ni kujengea uwezo jamii, ikaunguza athari za wanyamapori, kuwalinda wakulima na jamii dhidi ya matukio hayo na mipango endelevu ya ardhi inayozingatia mizania na utambuzi wa shughuli za kibinadamu.

Nyingine anaitaja, ni kuboresha maisha na kuwaelimisha Watanzania umuhimu wa kutumia rasilimali kwa namna jumuishi, pamoja na kufuatilia utafiti.

Anasema, mbinu zote zinalenga kuondoa mtazamo hasi dhidi ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa wananchi kufanya shughuli za kurina asali, uvunaji mapato yatokanayo na utalii na faida za uhifadhi.

Meneja Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, Dk. Elikana Kalumanga, anataja aina mbili za shoroba ni; za kutengenezwa na binadamu na za asili zinazolindwa na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009.

Anafafanua, kuna umuhimu wa kuhusisha sekta binafsi kutunza shoroba, kwa kuwa ziliachwa nyuma na ndio maana maeneo mengi yameshambuliwa na shughuli za kibinadamu.

Kwa mujibu wa Dk. Kalumanga, shoroba ni muhimu hifadhini kwa kuwasaidia wanyama kutembea kutoka eneo moja kwenda jingine kupata mahitaji muhimu kwa afya zao, wakiendeleza ikolojia. Hapo anataja ni pamoja na kuyafikia kirahisi maeneo yenye mtawanyiko.

Anasema, kutembea huko kunakamilisha ikolojia yao, wakifuata malisho na madini muhimu yanakopatikana, akitoa mfano wa wanyama nyumbu, wanaohama Hifadhi ya Taifa Serengeti kwenda Masaimara Kenya na baadaye wanarudi Serengeti kupitia kwenye shoroba zilizoko.

### FAIDA YA SHOROBA

Dk. Kalumanga anasema, faida ya shoroba ni kubwa, hasa kwa wananchi waishio jirani na hifadhi, akitoa mfano wa shoroba ya Kwakuchinja, inayounganisha Hifadhi ya Taifa Tarangire na Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara.

"Kwenye eneo hili wananchi wa vijiji 10 wametoa ardhi ili kuongeza eneo lililohifadhiwa, wanalilinda wenyewe na wanapata mengi yanayosaidia maendeleo yao, wana wawekezaji kwenye hoteli tano na eneo la uwindaji.

"Wananchi zaidi ya 200 wamepata ajira kutokana na uhifadhi wa shoroba na eneo hilo, kuna maduka 19 ya kuuza bidhaa za utalii, jumla ya watalii 33,151. Mwaka 2019 walitembelea Burunge kati yao wa ndani ni 8,020 na 25,131 ni kutoka nje ya nchi," anaeleza.

Anafafanua, kutokana na janga la maradhi UVIKO-19, idadi tajwa ilipungua hadi kufika10,919 mwaka 2020, kwa uwiano, Watanzania 3,881 na 7,038 ni wageni.

Dk. Kalumanga anasema, wananchi wanajishughulisha na kurina asali, pia wanavua kwenye Ziwa Burunge linalotumiwa na wanyama, binadamu na ufugaji mdogo.

Faida nyingine anaitaja ni wanyama kuendeleza kizazi. Anatoa angalizo la kuwapo hatari ya kujitokeza ugonjwa, pia wanyama kukimbia majanga ya moto, magonjwa, ukame na mafuriko, kwani hawaendi eneo jingine lililohifadhiwa.

Anasema, tishio kubwa la kupungua ukubwa wa shoroba husika kutokana na shughuli za kibinadamu, imechangiwa na watu kumefungua mashamba, majengo ya makazi ya kudumu, wanawinda wanyama, kushambuliwa na wanyama wakipita kwenye njia zao, uharibifu mkubwa wa mazingira na migogoro baina ya wanyama na binadamu.

### CHANGAMOTO

Mtaalamu wa Matumizi Bora ya Ardhi na Uhifadhi wa Bioanuwai USAID Tuhifadhi Maliasili, Joseph Olila, anasema kuna changamoto ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuwa kijiji kimoja.

Anashauri uwezekano wa kulitenga eneo husika kwa ajili ya kilimo, pia upande mwingine unakuwa malisho ya wanyama.

Katika kila kikao bungeni, kumekuwapo sauti za kulalamikia uharibifu wa mazao, watu kuuawa, pia kujeruhiwa na wanyamapori, wakiitaka serikali kuchukua hatua stahiki.

Akiahirisha Mkutano wa Bunge la Bajeti mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akasema serikali imetenga fedha ya kujenga vituo sita muhimu kwa ajili ya kuwafukuza wanyamapori wanapoyafikia maeneo ya wananchi.

AFYA

## MAHAFALI 20 YA HUBERT KAIRUKI….

# Yaipatia sekta afya madaktari 1,560



Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki wakiwa kwenye mahafali, mwaka jana. **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA ya afya nchini kitaaluma inakabiliwa na uhaba wa watumishi wake, kuanzia ngazi ya madaktari bingwa, wauguzi na watumishi wa kada zingine ndani ya sekta hiyo.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linapendekeza uwiano kati ya daktari na mgonjwa katika nchi kama Tanzania, iwe mmoja kwa wagonjwa 8,000.

Hadi sasa inaelezwa uwiano ulioko nchini, ni kila daktari anahudumia wagonjwa 20,000. Maana yake, kuna ziada ya wagonjwa 12,000 au mara mbili na nusu ya kile anachopaswa kuhudumia.

Mahitaji ya namna hiyo ya wataalamu, ni sababu mojawapo ya kuanzishwa vyuo vikuu binafsi, kusaidia jitihada za serikali kuzalisha wataalamu na wasomi wa sekta hiyo, kuziba pengo lililoko kwenye sekta nzima.

Hapo ndipo, Mtandao wa Elimu ya Afya Kairuki (KHEN), uliamua kuanzisha Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), lengo ni kuzalisha watumishi wa sekta ya afya.

### UONGOZI WA CHUO

Mwenyekiti wa KHEN, Kokushubira Kairuki, anasema sababu ya taasisi hiyo kuwekeza kwenye elimu ya juu kuanzia mwaka 1992, ni uhaba wa rasilimali watu katika sekta ya afya nchini.

Anasema katika mahafali ya kwanza yaliyofanyika mwaka 2003, wahitimu wa KHEN walikuwa 63, kati yao madaktari wanne na waliobaki wauguzi.

Mwenyekiti huyo anasema, katika mahafali ya 20 yaliyofanyika mwishoni mwa mwaka jana, kulikuwapo wahitimu 294, hivyo kukifanya chuo hicho kuchangia

> **“Mchango wa sekta binafsi katika elimu ya juu nchini ni mkubwa, hali inayodhihirishwa na serikali kutambua umuhimu wao kushiriki katika huduma ya eneo hilo.**

jumla ya rasilimali watu katika sekta ya afya 3,186, kati yao 1,560, idadi inayokabiria nusu (48.96%) ni madaktari wa binadamu.

Kokushubira anasema, mahitaji bado ni makubwa na wametoa mchango wao kwa taifa katika kupunguza uhaba wa rasilimali watu kwa miaka 25 mfululizo. Hapo anaiishukuru serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Teknlolojia, Wizara ya Afya na taasisi zingine za kiserikali.

Vilevile anawaingiza katika orodha mahsusi; Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), hospitali za umma na manispaa zinazoichangia KHEN kufika iliko sasa.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, John Ulanga, anatumia nafasi hiyo kuiomba serikali kuendelea kuongeza mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wa fani za afya, akiamini itapunguza uhaba wa watumishi kwenye sekta hiyo nchini.

Ulanga anasema chuo hicho kimetoa mchango mkubwa tangu kuanzishwa kwake, ikitoa wataalamu wa kada mbalimbali wa afya, wakiwamo madaktari bingwa waliosambaa nchini.

Mkuu wa Chuo hicho, Anne Makinda, anasema Chuo Kikuu cha Hubert Kairuki, tangu kuanzishwa kimejitahidi kutoa wahitimu bora na matunda ya kazi zao yanaonekana kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

“Hivi karibuni tulikuwa na kusanyiko la kitaaluma, walikuja waliowahi kusoma HKMU, kwa kweli ukiwasiliza wanavyowasilisha mada zao wanavyojiamini, unapata uhakika kabisa kwamba hapa ni sehemu sahihi ya kufundisha watumishi wa kada ya afya,” anasema Makinda.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Yohana Mashalla, anaomba serikali ipunguze gharama za vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili wanafunzi wengi zaidi waweze kusoma kwa njia ya mtandao.

Profesa Mashalla, pia anaiomba serikali kuvipa ruzuku vyuo vikuu binafsi, ili vijiandae kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu, kusomesha wahadhiri na ununuzi wa vifaa vya kufundishia, maabara na maktaba, wakidhi mahitaji ya kuongezekaa elimu ya juu nchini.

Anasema, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wahadhiri, HKMU imeendelea kufadhili masomo ya wahadhiri ngazi ya uzamili na uzamivu ndani na nje ya nchi.

Makamu Mkuu wa Chuo anasema, kwa sasa kuna wahadhiri 14 walioko masomoni, kati yao saba ngazi ya uzamivu na idadi kama hiyo wengine wako ngazi ya uzamili.

Profesa Mashalla anasema, mchango wa sekta binafsi katika elimu ya juu nchini ni mkubwa, hali inayodhihirishwa na serikali kutambua umuhimu wao kushiriki katika huduma ya eneo hilo.

Anafafanua kuwa, takwimu za serikali zinaonyesha tangu mwaka 1995, vyuo vikuu vimeongezeka kufikia asilimia 18, vyuo vikuu vishiriki 10 pamoja na vituo vitatu vya kufundishia (Campus Centers) mwaka wa masomo wa 2022/2023.

Kwa mujibu wa Profesa Marshalla, sekta ya afya kwa mwaka wa masomo wa 2021/2022, vyuo binafsi vilikuwa na wanafunzi 13,766, ikilinganishwa na wanafunzi 10,586 wa vyuo vikuu vya umma.

Pia, anaeleza kuwa nusu ya wahitimu wa programu za afya na sayansi shirikishi, wanatoka kwenye vyuo vikuu binafsi, hivyo anajigamba kuwa mchango wa KHEN katika kuzalisha wataalamu wa sekta ya afya iko juu.

Anasema hadi sasa, KHEN inafanya mawasiliano na ubalozi wa Tanzania nje ya nchi, kutafuta wataalamu wa afya wenye uwezo wa kufundisha na kushirikiana na wahadhiri katika tafiti, kwenye maeneo ya kimkakati.

“Ni matarajio yetu kuwa jitihada hizi zitaleta matunda na kuleta ufanisi katika ufundishaji, utafiti na utoaji wa huduma kwa wananchi,” anasema.

Katika kukabiliana na uhaba wa madarasa, anasema kwa mwaka wa masomo uliopita, waliweka viti kwenye kumbi za mihadhara kusaidia kuongeza nafasi za kufundishia na wakadahili idadi kubwa zaidi ya wanafunzi.

### DARASA KWA IT

Profesa Mashalla anataja pia mbinu mojawapo wanatumia, ni kupunguza uhaba wa madarasa kwa wakitumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano au TEHAMA, kwa kuongeza uwezo wa hadi mawasiliano (200MB/s) unaotumiwa na watumishi na wafanyakazi, mahali popote bila ya malipo.

“Hii ni juhudi za kukiimarisha chuo katika utumiaji wa TEHAMA katika shughuli zake zote muhimu na kwa kutumia mtandao chuo, kimepunguza ulazima wa mhadhiri kufundisha wanafunzi uso kwa uso,” anasema

Anaifafanua, ni hatua inayowezekana, baada ya TCU, kurasimisha ufundishaji kwa njia ya mtandao, mhadhiri anaweza kutumia mtandao kusahihisha mtihani na kutoa matokeo kwa wepesi, hata kama darasa lina wanafunzi wengi.

Ahadi yake ni kwamba, KHEN itaendelea kuwekeza kwenye mifumo ya TEHAMA, ili kutanua wigo wa ufanisi kufikia wanafunzi wengi.

### MAGUMU YA MIKOPO

Kuhusu mikopo kwa wanafunzi wa chuo cha KHEN, Profesa Mashalla anasema, baadhi ya wanafunzi wanashindwa kulipa ada kwa wakati na idadi ya wanaopata mikopo imeendelea kupungua.

“Hii imesababisha baadhi ya wanafunzi kupata kiasi kidogo cha mikopo kwa ajili ya malipo ya ada na wengi kukosa kabisa.

“Wapo wachache wanaopata mikopo kwa asilimia 100, lakini wakashindwa kuchangia kiasi kilichobaki, ili kufikia ada kamili,” ananena, akitaja sehemu ya magumu ya vyuo vikuu binafsi wanayopata katika shughuli zao.



## Wasomi vyuoni kufundisha afya shule za msingi, sekondari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeweka mkakati wa kuwatumia wanafunzi wanaosoma kozi za afya vyuo vya kati na vyuo vikuu kutoa elimu katika shule za msingi, sekondari na ngazi ya jamii.

Lengo likiwa ni kuhakikisha elimu ya afya inafika katika ngazi ya shule ya msingi na sekondari kwa ufasaha.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi (Elimu ya Afya kwa Umma, Idara ya Kinga, Wizara ya Afya), Dk.Tumaini Haonga, alibainisha hayo juzi katika warsha ya siku mbili ya 'afya day' iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha St.John's iliyoratibiwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Dk. Haonga alisema ili kuhakikisha elimu ya afya inafika kwa wakati shuleni ni muhimu sasa wanafunzi wa vyuo vya kati na vyuo vikuu wanaosomea kozi za afya wanatumika kutoa elimu kama sehemu ya mafunzo ya vitendo kwao.

"Mwanafunzi wa chuo kikuu anayesoma ngazi ya astashahada, stashahada na shahada kwenye eneo la afya muda wa kufanya mazoezi ni muhimu... Nitaelekeza wadau wa maendeleo kuongeza bajeti kuwezesha suala hili na liwe la utekelezaji Dodoma na nchi nzima kwa ujumla," alisema Dk. Haonga.

Aidha, Dk.Haonga alisema waandishi wa habari wana mchango mkubwa katika eneo la elimu ya afya kwa umma ili kuondoa dhana ya upotoshaji kwa jamii.

"Sisi tunawahitaji sana waandishi wa habari kwenye eneo la elimu ya afya kwa umma ili waweze kutusaidia kufafanua dhana potofu zinazoibuka kuhusu masuala ya afya zinazoweza kusababisha wananchi wasizingatie kanuni bora za afya,"alisema Dk.Haonga.

Ofisa Mpango wa Afya shuleni, Magdalena Dinawi, alisema kwa taratibu za nchi kijana anapimwa Virusi Vya Ukimwi kuanzia miaka 15 na kuendelea bila ridhaa ya wazazi wake.

Naye Mwenyekiti wa timu za uhamasishaji uchangiaji damu kanda ya kati, Dk.Leah Kitundya alisema mahitaji ya damu ni makubwa hivyo wananchi wanapaswa kuendelea kujitokeza kuchangia.

# Wamiliki shule za dini watakiwa kusimamia maadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKUU wa shule za sekondari zinazomilikiwa na taasisi za dini nchini wametakiwa kusimamia maadili ya wanafunzi na walimu ili kuwa na kizazi chenye maadili.

Msaidizi wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, Mchungaji Deogratius Msanya aliyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa wakuu hao ulioandaliwa na Kamisheni ya Huduma za Jamii ya Kikristo (CSSC).

Alisema jambo kubwa linalosumbua kwa sasa ni maadili kwa wanafunzi na walimu, hivyo kuna haja ya wakuu hao kupaza sauti ili kukomesha vitendo hivyo.

"Mtoto ambaye amejengwa kwenye misingi ya kiimani na kimaadili atakuwa vizuri na atakuwa na hofu ya Mungu na hata mahali pa kazi utaona utendaji kazi wake utakuwa ni wa hali ya kujali na ataonesha kuwajali wale anaowahudumia," alisema.

Alisema kama kuna mambo yasiyo mazuri ni vyema kuchukua hatua za haraka kushughulika ili kutokuwa na kizazi chenye shida baadaye.

Hata hivyo aliishauri serikali kutafuta ufumbuzi wa kero mbalimbali ambazo zinajitokeza katika jamii ikiwamo suala la ukosefu wa maadili na vitendo ambavyo havimpendezi Mungu.

"Changamoto naona ni utandawazi taarifa zipo kiganjani wanafunzi wanajifunza mambo mengi sana, watoto kuwapa simu wakiwa na umri mdogo nayo ni shida, ukweli tungependa sana shule zetu zisitajwe kwenye mambo kama hayo wakuu wa shule zetu angalieni elimu yenye maadili," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa CSSC, Peter Maduki, alisema taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 1992 kwa ajili ya kuimarisha huduma za utoaji wa elimu na afya zinazotolewa na taasisi za kanisa.

Alisema wana taasisi za elimu 1,033 ambazo zimesajiliwa na serikali katika ngazi ya elimu ya awali msingi, sekondari vyuo vya kati, ufundi na vyuo vikuu.

Alibainisha ili elimu iwe bora wanashughulikia suala la maadili kwa kufuata sera ya ulinzi wa mtoto na kufundisha elimu ya dini kwa wanafunzi na mafunzo ya kanuni za kazi na maadili kwa walimu ili kuhakikisha wanafunzi wanalelewa katika misingi ambayo wanatarajiwa na jamii.

Alisema wanajaribu kuimarisha mafunzo ya dini ili wanafunzi waishi kulingana na maadili na wanakuwa na upendo kuwaepusha kwenda kinyume na msingi wa kanisa.

"Tumenzisha klabu za ulinzi wa watoto shuleni ili waweze kuelimishana juu ya mambo hayo, wito wangu kwa jamii na wazazi, malezi lazima yahusishe jamii nzima malezi mazuri yanatolewa nyumbani wasiwaachie walimu peke yao," alisema Maduki.

Mkuu wa Idara ya Elimu Baraza la Maskofu Tanzania (TEC), Sista Joyce Mboya, alisema kupitia mkutano huo wamejifunza kuhusu malezi kwa vijana na watahakikisha shule wanazozisimamia kwa vitendo.

"Ndio maana sisi tuna sera inayotuongoza na tuna vitabu vya kufundishia ili wakienda popote waweze kufanya kazi wawe wawajibikaji na wabunifu kwa ajili ya kuendeleza taifa," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Seleman Jafo, akizungumza kwenye kikao cha Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ukimwona kijana huyu toa taarifa haraka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKAZI wa Nzuguni 'B' jijini Dodoma, Noel Nyau (33) (pichani), amepotea katika mazingira ya kutatanisha tangu Januari 20, mwaka huu, huku familia yake ikimtafuta katika maeneo mbalimbali bila mafanikio.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapo, baba mzazi wa kijana huyo, Mchungaji Steven Nyau alisema kuwa mtoto wake alipotea Januari 20 mwaka huu walipokuwa naye katika Kituo Kikuu cha Polisi.

"Siku hiyo tulikwenda naye polisi kwa ajili ya kumwekea dhamana mtoto wake ambaye ni mjukuu wangu polisi walimkamata kutokana na tukio lililotokea kule kwetu la uvunjaji kwenye mashine."

"Kutokana na polisi kukamata vijana wengi kwenye tukio hili walimkamata na mjukuu wangu ndiyo ikabidi twende kumwekea dhamana kituo cha polisi,"alisema Nyau.

Aidha, alisema wakiwa katika kituo hicho cha polisi kijana wake huyo alimwomba ruhusa atoke kidogo lakini alipoondoka hakurudi tena.

"Tukiwa pale polisi tunafuatilia dhamana aliniomba atoke kidogo lakini alipoondoka hakurudi tena nikajua labda kapata shida, kwa kuwa hakuwa na simu, siku mbili zilizopita nikaendelea na nilipomaliza nikarudi nyumbani kwangu sikumkuta wala kwake hakuwapo,"alisema.

Kadhalika, alisema baada ya kumkosa nyumbani aliamua kufuatilia katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwa marafiki zake lakini bila mafanikio.

"Baada ya kutafuta kila sehemu na kumkosa ikanibidi kurudi polisi na kutoa taarifa ambapo nilipatiwa RB namba DOM/RB/983/2023,"alisema.

Vile vile, alisema kijana wake siku ya tukio alivaa nguo za rangi ya bluu na shati la drafti.

Alisema: "Kwa atakayemwona sehemu yoyote tunaomba atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichoko karibu naye au apige simu namba **0762993332,**"alisema Mchungaji Nyau.







# Dk. Tulia atoa msaada wa bima za afya wananchi 3,000

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, amekabidhi msaada wa bima za afya kwa wananchi 3,000 wa Jiji la Mbeya wanaotoka kwenye familia maskini kwa lengo la kuwasaidia kupata matibabu wanapougua.

Baadhi ya makundi ya wananchi walionufaika na msaada huo ni wenye ulemavu, yatima na wazee ambao hawana uwezo wa kujimudu kulipia gharama za matibabu.

Dk. Tulia alisema ambaye ni Spika wa Bunge alisema mbali na kuwapatia bima hizo pia aliwanunulia viti mwendo baadhi ya wenye ulemavu, kuwakarabati nyumba baadhi ya wazee na kuwapatia mitaji baadhi ya walioonekana wakifanya biashara ndogo.

Alisema lengo la kuyasaidia makundi hayo ilikuwa ni kuyasaidia kupata huduma za matibabu kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya bila matatizo ya aina yoyote.

Alisema serikali imejenga miundombinu mingi ya kutolea huduma za afya lakini kama makundi hayo hayatakuwa na bima za afya yatashindwa kunufaika na miundombinu hiyo.

"Watu 3,000 wanaonekana ni wengi na tukio la leo linaonekana kuwa ni kubwa lakini kiuhalisia hapa Mbeya Mjini bado watu wanaohitaji ni wengi sana, watu wasiokuwa na uwezo ni wengi na hivyo tunatamani tuendelee kuwasaidia na wengine," alisema Dk. Tulia.

Aliwataka wananchi wenye uwezo wa kujilipia huduma hiyo waanze kujipanga kwa ajili ya kupata bima wakati serikali itakapokamilisha mchakato wa bima ya afya kwa wote.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala, alisema bima hizo ambazo wananchi hao walipatiwa zinatumika katika ngazi mbalimbali za vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema zinatumika kuanzia katika ngazi ya zahanati mpaka katika Hospitali ya Mkoa na hivyo akamshukuru Dk. Tulia kwa kuyasaidia makundi hayo ambayo yamekuwa yakipata shida.

"Hizi bima siyo kwamba zitatumika katika Mkoa wa Mbeya pekee hapana, zitatumika nchi nzima kwa hiyo popote utakapokuwapo ukiugua unaweza ukaenda kwenye kituo chochote cha kutolea huduma na ukahudumiwa," alisema Dk. Lulandala.

Aliwataka wanufaika wa bima hizo kuzitumia wao wenyewe badala ya kuanza kuwapatia na watu wengine ili wakatibiwe kwa maelezo kuwa ni kosa ikibainika.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema ili kumuenzi Dk. Tulia kwa maendeleo ambayo anayafanya jijini Mbeya, Daraja la Mwasanga litapewa jina lake ili iwe miongoni mwa kumbukumbu muhimu kwake.

Aliwataka wanasiasa wa Jiji hilo kumuunga mkono kiongozi huyo badala ya kuendeleza misigano ambayo alieleza kuwa haina maana kwa wananchi wa jiji hilo.

Alisema katika Jiji hilo kuna tatizo la baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwa wakibaguana kutokana na tofauti zao za kikabila jambo ambalo alisema halina maana.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na Dk. Tulia katika shughuli mbalimbali za maendeleo ambazo amekuwa akizifanya na kuhamasisha ili afikie malengo yake ya kuwahudumia.

Baadhi ya wanufaika wa bima hizo walisema zitawasaidia kupata matibabu kwa urahisi wakieleza kuwa wakati mwingine walikuwa wanashindwa kuhudumiwa kwa sababu ya kukosa fedha.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akikabidhi kadi ya Bima ya Afya kwa mmoja kati ya wananchi 3,000 jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima wa tumbaku wailalamikia kampuni kutowalipa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKULIMA wa tumbaku wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wamelalamikia kampuni iliyokopa mazao yao msimu uliopita na kushindwa kuwalipa jambo ambalo linawafanya baadhi yao kukosa mtaji wa kulimia mwaka huu.

Aidha, wakulima hao wanadai kuwa licha ya kampuni hizo kutowalipa fedha zao lakini yamepewa tena tenda ya kuwasambazia pembejeo msimu huu na yanataka yalipwe.

Wakulima hao walitoa malalamiko hayo juzi kwenye Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU), walisema wana wasiwasi kampuni hizo zinaweza zikawadhulumu fedha zao.

Mmoja wa wakulima hao, John Kamuga alitaja kampuni wanayoidai kuwa ni Mo Green LTD ambayo ndiyo iliyopewa tena zabuni ya kuwasambazia dawa za kuzalishia zao hilo.

Alisema kampuni hiyo imesambaza dawa kwenye vyama vya msingi ambavyo vinaidai na inataka kulipwa fedha za dawa hizo wakati bado na wao wanaidai.

Aliiomba serikali kuwaweka kizuizini viongozi wa kampuni hiyo mpaka watakapowalipa wakulima ili kuwasaidia kuendelea na shughuli za uzalishaji wa zao hilo.

Naye Simon Ngomongo alitaja kampuni nyingine ambayo wanaidai kuwa ni Grant LTD ambayo imepewa tenda ya kuwasambazia wakulima mbolea lakini baadhi ya mbolea muhimu haijawapelekea.

Alisema kwa sasa mazao yao yanahitaji zaidi mbolea aina ya CAN lakini mpaka sasa hawajapelekewa na hawajui watapelekewa lini jambo ambalo alisema linaweza likasababisha uzalishaji kushuka ilikinganishwa na miaka mingine.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mbeya, Richard Zengo, aliwashauri wakulima hao kulipa fedha hizo kupitia Taasisi ya Usimamizi wa Ununuzi wa pembejeo kwenye vyama vikuu vya ushirika nchini (TCJE).

Aliwashauri wakulima hao kukubaliana na TCJE kuzitaka kampuni hizo fedha wanazodai ili zirejeshwe kwenye vyama vya msingi kisha zipelekwe kwa wakulima.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Usimamizi wa Ununuzi wa Pembejeo kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika nchini (TCJE), John Ntezilyo ambaye ndiye aliyeingia mikataba kampuni hizo alisema mikataba yao iko wazi na wakulima watalipwa.

Alisema kipo kipengele kwenye mikataba hiyo ambacho kinaelekeza kampuni yoyote ambayo inadaiwa na wakulima kukatwa sehemu ya fedha zake ili kuwarejeshea wakulima.

Aliwataka wakulima hao kuwa na imani na taasisi hiyo kwa maelezo kuwa itahakikisha wanawalipwa fedha zao ili waendelee na shughuli zao za kilimo.

# TARI yaanza utafiti wa mahindi lishe kukabili udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, kimeanza kufanya utafiti wa mahindi lishe (mahindi ya njano) ili kusaidia wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kukabiliana na udumavu.

Mtafiti wa mahindi katika kituo hicho, Leonald Sabula, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipasha kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi hiyo hasa utafiti wa mbegu za mazao.

Alisema walianza kufanya utafiti huo mwaka juzi na wanatarajia kutoa matokeo ya awali mwaka huu baada hasa katika kipindi cha maonyesho ya wakulima.

Alisema wanakusudia kukamilisha utafiti huo mwakani na kuanza kusambaza mbegu hizo kwa wakulima ili zianze kulimwa kwenye maeneo ambayo watabaini kuwa yanafaa kuzalishwa.

"Kwa sasa tunapambana zaidi na tatizo la udumavu hasa kwa watoto, haya mahindi yamebainika kuwa yana virutubisho vingi ambavyo vinafaa kwa watoto kwenye mikoa yetu hii," alisema Sabula.

Sabula alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inazalisha chakula kwa wingi lakini ndiyo inayokabiliwa na udumavu kwa kiwango kikubwa.

Alisema mbali na mahindi hayo, pia kituo hicho kinazalisha mazao mengine yenye virutubishi muhimu kwa watoto ikiwamo viazi lishe na maharage.

Alisema mazao hayo yote yanatakiwa kuliwa na watu wote bila kujali umri huku akisisitiza kuwa ni muhimu zaidi kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Hata hivyo Sabula alisema mahindi hayo yana soko kubwa duniani ambalo Watanzania wanatakiwa kuchangamkia kuzalisha hasa katika nchi ya Misri.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa chakula na inajulikana kama ghala la taifa la chakula lakini inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wenye udumavu.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Fimbo Butallah, akitambulisha rasmi paketi mpya ya Bwana Sukari yenye ujazo wa gramu 50 itakayouzwa kwa bei ya 200/- tu, katika uzinduzi viwanja vya Mawenzi Sokoni, mjini Morogoro mapema wiki hii ili kuleta unafuu kwa watumiaji wa mwisho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 819 wenye mahitaji maalum wafanya mtihani wa taifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI 819 wenye mahitaji maalumu wamefanya mitihani yao ya taifa mwaka 2022 hatua ambayo imeonyesha mafanikio makubwa katika sekta ya elimu Zanzibar kufikia malengo ya elimu kwa wote.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhamed Mussa, aliyasema hayo jana wakati alipozungumza na watendaji wa sekta ya elimu.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya mageuzi ya sekta ya elimu yanayotarajiwa kuendelea kutekelezwa nchini kote yakiwamo kuimarishwa kwa miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Alisema mageuzi hayo yanakwenda sambamba na ujenzi wa shule mbili za kisasa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu huko Pujini katika Kisiwa cha Pemba pamoja na Jendele Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu nchini kote ni sehemu ya utekelezaji wa malengo endelevu ya dunia ambapo suala la elimu kwa wote limetajwa.

"Ninachoweza kusema Wizara ya Elimu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza malengo endelevu ya dunia ya kuona wanafunzi wanafikiwa na elimu katika makundi yote".

Akitangaza matokeo hayo mbele ya waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani la Zanzibar, Othman Omar Othman, alisema katika matokeo hayo yanaonyesha Wizara ya Elimu imefanya mageuzi makubwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambapo jumla ya wanafunzi 819 wamefanya mitihani ikiwamo wenye uoni hafifu pamoja na viziwi.

Alisema ufaulu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu unaridhisha kwa kiwango kikubwa ambapo mafanikio hayo yanatokana na shule zinazotumiwa kuwa na vifaa kamili kwa mahitaji yao.

Aliwataja watahiniwa wenye mahitaji maalumu waliosajiliwa kufanya mitihani hiyo ni pamoja na wenye ulemavu wa akili, walemavu wa viungo na walemavu mchanganyiko na wale ambao hawaoni kabisa wanaolazimika kutumia vifaa maalumu.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, alisema katika mpango wa mageuzi makubwa ya sekta ya elimu yanayotarajiwa kutekelezwa mwaka huu suala la elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu limepewa kipaumbele cha kwanza ili kwenda sambamba na mikakati pamoja na mikataba ya kimataifa ya haki za watu wenye ulemavu katika kupata elimu.

Alisema shule mbili kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu zimejengwa Unguja na Pemba ambazo zitakuwa na vifaa kamili kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kufanya kazi za vitendo na ujuzi.

# Majaji, mahakimu watakiwa kutoa hukumu kwa Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAJAJI wa Mahakama Kuu ya Zanzibar pamoja na mahakimu wametakiwa kutoa mwenendo wa hukumu kwa lugha ya Kiswahili ambayo itawasaidia na kuwawezesha watuhumiwa kukata rufani baada ya kutoridhishwa na mwenendo wa hukumu walizopewa.

Hayo yalisemwa jana na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla, alipofanya ziara ya kutembelea Magereza na kufanya mazungumzo na wafungwa wanaotumikia vifungo mbalimbali visiwani humo. Alisema mwenendo wa hukumu inapotolewa kwa lugha ambayo mtuhumiwa anaitumikia vizuri inamwezesha kujua mwelekeo ikiwamo kukata rufani baada ya kutoridhishwa na mwenendo mzima wa kesi hiyo.

Alisema baadhi ya watuhumiwa wanashindwa kukata rufani kwa sababu hawafahamu mwenendo mzima wa kesi yake pamoja na hukumu ambayo imetolewa kwa lugha ya Kiingereza.

Mrajisi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Valentina Andrew Katema, alisema mahakama kwa sasa ipo katika kipindi cha maboresho makubwa ikiwamo katika usikilizaji wa kesi na mwenendo wake kwa ujumla na mahakimu wake.

Katema aliwataka mahakimu kuongeza kasi ya kusikiliza kesi zinazofikishwa na kutochukuwa muda mrefu katika kutoa maamuzi yake kwa lengo la kuepusha malalamiko yalioko awali.

Aidha, aliyataja maboresho mingine yaliyofanywa ikiwamo kutoa ajira zaidi kwa majaji na mahakimu wapya hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kesi kusikilizwa na kutolewa hukumu katika kipindi kifupi.

Alisema Mahakama imeimarisha mahusiano yake ya kufanya kazi kwa karibu na vyuo vya mafunzo magereza pamoja na Jeshi la Polisi ambapo taasisi hizo zinafanya kazi kwa karibu katika masuala ya sheria na kufuatilia mwenendo wa kesi. Uongozi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar ukiongozwa na Jaji Mkuu wa Zanzibar ulifanya ziara katika magereza ikiwamo gereza kuu lilioko Kinua Miguu Unguja na kupata nafasi kusikiliza malalamiko mbalimbali kutoka kwa wafungwa ambao wanatumikia adhabu mbalimbali.

# 'SMZ inathamini mchango wa wadau kukuza sekta ya afya'

**Na Mwandishi wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman, amesema Serikali ya Zanzibar inathamini juhudi za wadau wa maendeleo katika kukuza sekta ya afya nchini.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa mapitio na kujadili mpango mkakati wa utekelezaji wa sekta ya afya Zanzibar.

Alisema mafanikio yanayopatikana nchini yamechangiwa na juhudi za washirika hao wanaoendelea kuunga mkono na kusaidia katika kufikia malengo kwenye sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya afya.

Hemed alisema ajenda ya mkutano huo inakwenda sambamba na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha inakuwa na mpango imara katika kutoa huduma bora na endelevu kwa wananchi wake.

Alisema kupitia mpango huo serikali imeona umuhimu mkubwa wa kuanzisha mfuko wa fedha wa huduma za afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya kwa haraka na urahisi na kutoa wito kwa watendaji wa mfuko huo kuhakikisha fedha zitakazokusanywa zikatumike kama zilivyokusudiwa ili wananchi wapate huduma endelevu za afya kwa wote.

Alisema serikali imechukua jitihada za makusudi kwa kujenga hospitali katika kila wilaya ili kuhakikisha panakuwa na mazingira mazuri ya kutekeleza mikakati ya kukuza sekta ya afya.

Aidha, alisema kuwa serikali itahakikisha mahitaji yote ya lazima yanapatikana katika hospitali hizo na kueleza kuwa mpango wa serikali ni kujenga hospitali katika mikoa yote ya Zanzibar.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kuwa juhudi zinazochukuliwa na serikali ni za kupigiwa mfano na kuahidi kuwa matatizo ya upungufu wa madaktari na watoaji wa huduma za afya inafanyiwa kazi ili kuhakikisha vituo vyote vya afya na hospitali kuna wataalamu wanaohitajika.

Aidha aliwataka wazazi kuwahimiza vijana kusomea fani ya udaktari bingwa ili kusaidia katika kumaliza changamoto hiyo.

Mwenyekiti wa Washirika wa Maendeleo, Dk. Alice Christensen, alisema kuwa mkutano huo utasaidia kufahamu maeneo muhimu ya kusaidia katika sekta ya afya pamoja na kujua hali ya afya kwa ujumla ndani ya Zanzibar.

Alisema kuwa sekta binafsi zinasaidia katika sekta ya sfya ili kupambana na maradhi hususani ya kuambukiza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA SHAMBA

Ndugu **MASOUD SULEIMAN NZOWAH** anatangaza kupotelewa na hati ya shamba **(HATI MILIKI NA.248 GM/534)** kilichopo mkoa wa wa **BAGAMOYO** –kiwangwa Kijiji cha **BAGI,** kwa yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/404102/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICENT ANYHONY KAWILIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina **SUZANE PATRICK** namba za usajili **T708AXP** aina ya Toyota **RAV 4.** Chassis No. **SXA117131101,** Engine No. **3S9385334.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/8911/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PAMELA WILFRED KIIZA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 622 CWX – TVS.** Chassis namba **MD625AF45MICI0082.** Engine namba **DF4CMIX09884.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/35275/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAKUNGILE COMPANY LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SUZUKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 962 BNL.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI **KAH /RB/ 49 /2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALTEMIUS THOBIAS MAPUNDA** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari (CATTLE) yenye usajili wa namba **T423 BWN** .Kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi au piga simu namba **0687742834.** **DSM/PHQ/RB/29455/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GEOFREY GEOFREY** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SUNLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 979 BEX .** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI KAH /RB/ 48 /2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FAUSTINA A. ANDREA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0774-0018 kilichotolewa na baraza mitihani la taifa kupitia LUPA SECONDARY SCHOOL mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/30002/2023**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701

## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED, JADA INVESTMENT LIMITED na MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED,** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MAGORI MWITA CHACHA | GHATIS NESPHORY | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI/ HATI NO 00332. | YANGEYANGE, KATA YA MSONGOLA, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM. | 11/02/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 2 | JAMILA M. YAHYA | ATHUMANI MUHIDINI | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA. TMK015576 | MAKANGARAWE BUZA, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 04/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 3 | SAID M MNG'ANGI | AFSA JABIRI MATIMBWA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK040637 | MBAGALA KIBURUGWA, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 25/03/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 4 | ABDALLAH H JUMA. | ZUHURA ALLY LIUKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK0451556 | CHARAMBE –RANGI TATTU, WILAYA YA TEMEKE | 15/04/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 5 | JOYCE G MWASABWITE | GWALUGANO OBASI MWASABWITE | KIWANJA NA. 34098PLOT NA 304 | MBAGALA KUU,MAGHARIBI, WILAYA YA TEMEKE | 06/05/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKER LIMITED |
| 6 | CECILIA MYEJI | SHEDRACK MAILO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.ILA/UKG/GLL4/58 | UKONGA GULUKA KWALALA, WILAYA YA ILALA | 27/5/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKER LIMITED |
| 7 | HAFSA ABDALLAH MUSHI | HAFSA ABDALLAH MUSHI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | LUIS MBEZI, MANISPAA YA KINODONI, DAR ES SALAAM | 11/2/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 8 | ABDALLAH HAJI NOMBOLE | ZABIBU MWAMEDI MBONDE | KIWANJA CHENYE LESENI YA MAKAZI TMK036432,PARCEL NO.TMK/MBGL/KNY28/157 | MBAGALA KWANYOKA, MANISPAA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 18/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 9 | ASANTE LOCKEN ANAEL | TRIPHONE GAMA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MBEZI SALASALA, MANISPAA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 25/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 10 | SHAIBU MUSA ROMBOLO | SHAIBU MUSA ROMBOLO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | CHAMANZI MSUFINI ,WILAYA YA TEMEKE DAR ES SALAAM | 17/02/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
| 11 | MWAJUMA C. MAGORI | ASIA ALLY GUBU | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI TMK044036,PARCEL NO.TMK/CHB/NZSA21/274A | NZASA A, C WILAYA YA TEMEKE | 10/02/2023,4:OO ASUBUHI NAKUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
| 12 | THOMAS AINAMEN MCHAU | THOMAS AINAMEN MCHAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MPONDA MIANZINI, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 17/02/2023: SAA 6: 00 MCHANA NAKUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
| 13 | YUSUPH RAMADHAN MCHOME | YUSUPH RAMADHAN MCHOME | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MBAGALA KUU, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 23/02/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
| 14 | JOYCE C MUSIBA | ELIAS THOMAS | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | CHANIKA LUKOONI, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 02/03/2023,SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
| 15 | AYUBU J AYUBU | AYUBU J AYUBU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BOKO CHAMA,WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 09/03/2023, SAA 4:00 ASUBUH NAKUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED | JADA INVESTMENT LIMITED | MBUZAX AUCTION MART & COMPANY LIMITED |
|---|---|---|
| P. O. Box 62163<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0658100737, 0757276263<br>Email: amazauctionma@gmail.com | P. O. Box 69098<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0788493699, 0768085727 | P. O. Box 62070<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0755506970, 0716763571 |

217245102

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Russia yaionya Marekani kuhusu vifaru

**MOSCOW,** Russia

RUSSIA imeonya Marekani kwamba vifaru aina ya Abrams vinavyopelekwa Ukraine, havitafika salama kwani vitashambuliwa kama vifaru vingine.

Msemaji wa nchi hiyo, Dmitry Peskov, alisema kwamba hatua hiyo ya Marekani kupeleka zana kwenda Ukraine, haitawasumbua kwa sababu wataalamu wanaojua vifaru hivyo wanafanya kazi.

"Ni kwamba upande wa teknolojia, huu ni mpango uliooshindwa na muhimu zaidi ni kukadiria wazi uwezo ambao utaongeza kwa vikosi vya kijeshi vya Ukraine. Huu ni udanganyifu mwingine mbaya sana," aliwaambia waandishi wa habari jana.

**Tumesema mara kwa mara kwamba vifaa kama hivyo havitabadilisha chochote, lakini vitaongeza matatizo kwa Ukraine na kwa watu wa Ukraine.**

Alisema mamlaka ya Russia inashirikisha wataalamu, kukabiliana na aina hiyo ya vifaa.

Awali, Peskov alizungumza kuhusu upelekaji wa vifaru aina ya Leopards kutoka Ujerumani.

"Tumesema mara kwa mara kwamba vifaa kama hivyo havitabadilisha chochote, lakini vitaongeza matatizo kwa Ukraine na kwa watu wa Ukraine," alisema wiki iliyopita.

Wakati huo huo, wataalamu wa nchi za Magharibi, wanaamini kwamba vifaru vizito vya Ujerumani na Marekani, pamoja na Challenger-2 ya Uingereza, itaruhusu vikosi vya Ukraine kuwafukuza wanajeshi ya Russia hadi nje ya mipaka.

Utawala wa Kijeshi wa Mkoa wa Luhansk, unadai kwamba Russia imeanza kusajili wanaume wa Ukraine ambao awali walifukuzwa kutoka maeneo yaliyokaliwa ya Ukraine.

"Wanaume waliofukuzwa kutoka maeneo yaliyokaliwa kwa muda wanasajiliwa kama wanajeshi kwenye eneo la Russia. Hii ni moja ya sababu za uamuzi uliochukuliwa na serikali ya Russia kutoa hati za kusafiria na mahali pa kuishi," alisema kiongozi mmoja.

Usajili huo unafanyika eneo la Krasnodar na kuratibiwa na kundi la Wagner.

Wakati huo huo, Raia wa Uingereza Chris Parry na Andrew Bagshaw, ambao waliripotiwa kutoweka mashariki mwa Ukraine, imefahamika kwamba wameuawa.

Kulingana na taarifa kutoka kwa familia zao, Bagshaw (47) na Parry (28), walionekana mara ya mwisho wakielekea katika jiji la Soledar Januari 6, mwaka huu.

Familia ya Bagshaw ilisema kuwa wawili hao walifariki wakati wakijaribu kumwokoa mwanamke mzee wakati magari yao yalipshambuliwa.

Familia ya Parry ilithibitisha watu hao walifariki walipokuwa wakijaribu kuwahamisha watu.

Mapema mwezi huu, kundi la mamluki la Wagner lilidai kuwa mwili wa mmoja wa watu hao ulikuwa umepatikana.

Soledar ilikuwa kitovu cha mapigano makali na mapema mwezi huu, jeshi la Russia lilidai kuuteka mji huo wa Ukraine ambao una mgodi wa chumvi.

Wakizungumza kumhusu Parry, mwenye asili ya Truro huko Cornwall, walisema kujitolea kwake kusaidia wazee, vijana na wasiojiweza huko kumefanya familia yake kuwa na fahari kubwa. **BBC**

## Somalia yapiga hatua kujiunga EAC

**MOGADISHU,** Somalia

NCHI ya Somalia imepiga hatua katika azma yake ya kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kama mwanachama wa nane.

Jumuiya ya wafanyabiashara wa kikanda jana imeanza zoezi la uhakiki ili kutathmini utayari wa nchi hiyo kupokelewa katika jamii.

Wataalamu kutoka nchi saba wanachama wa EAC, watakuwa mjini Mogadishu kwa muda wa wiki moja ijayo ili kubaini kiwango cha nchi hiyo cha kuzingatia vigezo vya kuandikishwa kwenye umoja huo.

Viongozi hao wakuu kutoka nchi za Kenya, Sudan Kusini, Rwanda, Burundi, Uganda, Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) watafanya tathmini ya mifumo ya kisheria ya Somalia, sera, mikakati ya maendeleo, miundombinu, amani na usalama pamoja na mambo mengine.

Kufuatia kukubaliwa kwa DRC mwaka jana katika umoja wa kikanda, Somalia imekuwa na nia ya kujiunga na EAC ikisema haitaki kuwa mzigo lakini inataka kuchangia vyema katika umoja huo kupitia biashara, kilimo, uchumi wa bluu na sekta nyinginezo.

Nchi hiyo ya Pembe ya Afrika ilitoa ombi la kujiunga na EAC mwaka 2012 bila mafanikio.

Rais Hassan Sheik Mohamud, alizindua ombi jipya Julai 2022 wakati wa mkutano wa kilele wa EAC nchini Tanzania ambako alialikwa kama mgeni maalum.

Baada ya kukamilika kwa hakiki, ripoti ya matokeo itawasilishwa kwa Baraza la Mawaziri la EAC ambao watawasilisha mbele ya wakuu wa nchi kwa ajili ya kuzingatiwa wakati wa mkutano wa kilele unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa Februari 2023. **BBC**



Ndege ya mafunzo ya Jeshi la Wanahewa la Ufilipino ilianguka kwenye shamba katika mji wa Pilar, mkoa wa Bataan. **PICHA: AFP**

## Ndege vita ya DRC yadaiwa kuingia Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

SERIKALI ya Rwanda imesema ndege ya kivita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imekiuka sheria na kuingia katika anga yake hapo jana.

Msemaji wa serikali ya Rwanda Yolande Makolo, alisema ndege ya kivita aina ya Sukhoi 25 kutoka Congo iliingia katika anga yake kwa mara ya tatu, kupitia Rubavu karibu na mji wa Goma na hatua za kujilinda zikachukuliwa, huku akiitaka DRC kuacha kuichokoza nchi hiyo.

Hata hivyo DRC imekanusha kuwa moja ya ndege zake imeingia katika anga ya Rwanda, na kulituhumu moja kwa moja taifa hilo kuishambulia ndege yake na kuliita tukio hilo kama hatua ya kuanzisha vita. **DRC**

## Mshirika wa Khan akamatwa Pakistan

**LAHORE,** Pakistan

POLISI nchini Pakistan imesema mshirika wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Imran Khan, amekamatwa kwa makosa ya kuwakashifu maofisa wa uchaguzi.

Fawad Chaudhry, aliyekuwa Waziri wa Habari chini ya utawala wa Khan, alikamatwa usiku wa kuamkia jana nyumbani kwake mjini Lahore.

Anashutumiwa kwa kuwanyanyasa na kuwatisha maofisa wa tume ya uchaguzi pamoja na familia zao, hiyo ni kulingana na ripoti ya polisi iliyosambazwa na chama chake cha Tehreek-e-Insaf.

Chaudhry, pia anadaiwa kuzuiliwa chini ya sheria ya uchochezi kwa sababu alijaribu kusababisha mkwamo katika mchakato wa uchaguzi.

Serikali ya Khan iliondolewa kwa kura ya kutokuwa na imani mwezi Aprili mwaka 2020 baada ya washirika wake katika serikali ya muungano kuacha kumuunga mkono.

Uchaguzi mpya unatarajiwa kufanyika kabla ya mwezi Oktoba, huku Pakistan ikiendelea kudidimia katika mgogoro wa kisiasa na kiuchumi.**DW**

# HABARI MICHEZO


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inatarajia kufanya Mnada wa hadhara wa vifaa chakavu mbalimbali vya ofisi kwa njia ya Mtandao. Mnada huo utafanyika siku ya Alhamisi ya tarehe 09 Februari, 2023 kuanzia saa sita na dakika moja (06.01) usiku hadi saa saba kamili (07:00) mchana.

Ili kushiriki Mnada huo, tembelea tovuti ya TRA ambayo ni **https://www.tra.go.tz.** kuanzia tarehe **26 Januari, 2023** ili kuona bidhaa zitakazouzwa.

Aidha, wanunuzi wanaweza kufika katika vituo vyenye bidhaa vilivyopo katika Mikoa ya Kodi ambavyo ni **Kigoma, Morogoro, Manyara, Pwani, Ruvuma, Mwanza, Katavi, Njombe, Mtwara, Kagera, Kilimanjaro, Lindi, Simiyu, Dodoma, Kahama, Tabora, Shinyanga, Pemba, Temeke, Kinondoni, Ofisi za Walipa Kodi Wakubwa (LTD) iliyopo katika jengo la Hazina - Dar es Salaam na Maghala ya TBA yaliyopo katika ofisi za TEMESA - Keko.**

**MASHARTI YA MNADA PENDEKEZWA**

1. Bidha itauzwa kama ilivyo mahali ilipo.
2. Malipo yote yatakuwa kwa fedha taslimu ambapo malipo ya awali ya kiwango cha asilimia 25 kitalipwa ndani ya saa 24 kulingana na taratibu za uendeshaji wa minada. Kiwango cha asilimia 75 kitalipwa ndani ya saa 48. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi na malipo ya awali yaliyolipwa hayatarudishwa.
3. Mnunuzi atalazimika kuondoa vifaa chakavu ndani ya siku tatu (3) baada ya kukamilisha malipo ya asilimia 100.
4. Ruhusa ya kuangalia vifaa imetolewa kwa siku kumi nne kabla ya tarehe ya Mnada.
5. Mnada utaanza siku ya tarehe 09 Februari, 2023 saa sita na dakika moja (06:01) usiku na kuisha siku hiyohiyo saa saba kamili (07:00) mchana.
6. Vigezo na masharti kuzingatiwa.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na**
**Kamishna Mkuu**





Mkuu wa Kitengo cha Thamani kwa Wateja wa Kampuni ya MultiChoice Tanzania, Hilda Nakajumo, akionyesha kauli mbiu ya kampeni mpya ya 'Panda Tukupandishe' kwa ajili ya wateja wao kupata burudani ya mechi na filamu zaidi iliyozinduliwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *DSTV na Panda Tukupandishe*

**Na Mwandishi Wetu**

DSTV Tanzania imetangaza promosheni mahususi kwa wateja wake ambapo kwa kipindi cha miezi miwili itakuwa ikiwapandisha vifurushi wateja wake.

Promosheni hii inawawezesha wateja wa DStv wanaokidhi vigezo, wateja wanaoendelea na wateja wapya kupata fursa ya kulipia kifurushi kinachofuatia cha juu yake na kupandishwa kwa kupatiwa kifurushi cha juu ya kile walicholipia kwa muda wa mwezi mmoja.

Promosheni hii inawahusu wateja wote wa vifurushi vya DStv vya Poa, Bomba, Shangwe na Compact ambapo watakapolipia kifurushi cha juu ya kile wanachotumia watapandisha zaidi na kuwashiwa kifurushi cha juu ya kile walicholipia kwa kufurahia maudhui ya kifurushi cha juu kwa mwezi mzima bila gharama ya ziada.

"MultiChoice Tanzania inafurahi kuzindua rasmi promosheni yake maalum ya 'Panda tukupandishe' hii ikiwa ni njia mojawapo ya kuwatunuku wateja wetu kwa kuendelea kuwa nasi na pia njia ya kuwahakikishia tumejipanga vyema kuendelea kuwapatia burudani isiyo na kifani," alisema Hilda Nakajumo, Mkuu wa thamani kwa wateja wa MultiChoice Tanzania wakati wa uzinduzi rasmi wa promosheni hiyo jijini Dar es Salaam jana.

Alisema kampuni hiyo inaendelea kuwapatia wateja wake burudani ya kina bila kusahau maudhui mengine kama habari na elimu, huku ikihakikisha wateja wake wanapata maudhui kemkem na ya kusisimua ya ndani na nje.

Aliongeza mteja wa DStv anayelipia kifurushi cha juu ya kile anachotumia au cha mwisho kutumia atapandishwa kifurushi kwa muda wa mwezi mmoja bila malipo ya ziada na pia mteja mpya wa DStv aliyejiunga siku au baada ya tarehe Januari 5, mwaka huu, ambaye atalipia kifurushi cha juu ya kile alichojiunga nacho naye pia atanufaika na ofa hii.

Hata hivyo, wateja wa DStv ambao wamelipia kifurushi chao kwa mwaka mzima hawahusiki na promosheni hii kwani hawa tayari wana ofa yao ambapo hupata mwezi mmoja wa kifurushi chao bila malipo ya ziada.


## BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD

**WE ARE DEALING GENERAL AUCTIONING, DEBT COLLECTION, EVICTION, INVESTIGATION AND REPOSSESSION, STORAGE, COMMISSION AGENCY AND GENERAL BUSINESS.**
**(MABINGWA WA KUKUSANYA MADENI SUGU)**

## NOTISI YA SIKU (14) NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **STANBIC BANK TANZANIA LIMITED** tunapenda kukutaarifu mdaiwa sugu kuwa unatakiwa kulipa deni unalodaiwa na mteja wetu kwamba unatakiwa kulipa deni hilo ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili.Pia tumeelekezwa kuwa ukishindwa kulipa deni hilo ndani ya siku 14 tutauza kwa mnada wa hadhara mali iliyowekwa dhamana ambayo ni kama ifuatavyo;

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAELEZO YA DHAMANA | ENEO LA MNADA | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|
| CHARLES CHABRUM A LUHWAVI | GARI | T 617 DTV FORD PICK UP | Mnada utafanyika kwenye ghala la BILO STAR LILILOPO MBEYA | Tarehe 18/02/2023 kuanzia saa nne asubuhi na kuendelea . |

**MAELEZO YA GARI:** Ina hati halali (KADI HALISI)

1172444302

**MASHARTI YA MNADA.**

Mnunuzi atakayefanikiwa kununua gari husika atalazimika kulipa 25% papohapo, na kiasi kilichobaki 75% atatakiwa kulipa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Akishindwa kulipa 25% aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa tena.

**KWA MAELEZO ZAIDI**

**Fika ofisi zetu zilizopo Mbezi Beach au wasiliana nasi kwa simu namba 0716 943424, 0719 206984, bilostarcompany@gmail.com.S.L.P 16095, DAR ES SALAAM.**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**EVERTON YAWEKWA SOKONI**

EVERTON imewekwa sokoni na inauzwa kwa bei ya pauni milioni 500, hata hivyo mmiliki, Farhad Moshiri, amekanusha taarifa za uwezekano wa kuuzwa, akisisitiza amejitolea kuitumikia klabu hiyo inayokabiliwa na matatizo na hatari ya kushuka daraja. ***(Liverpool Echo)***

**ARSENAL, CHELSEA VITANI**

ARSENAL inaweza kushindana na Chelsea katika kumnunua kiungo wa kati wa Brighton, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21 msimu wa joto. ***(Evening Standard)***

**BIELSA ATAJWA EVERTON**

KLABU ya Everton itaendelea na mazungumzo na Marcelo Bielsa kuhusu kocha wao mpya, lakini watafikiria kumteua bosi wao wa zamani, Sam Allardyce. ***(Independent)***

**HARRISON ANUKIA LEICESTER**

WINGA wa Leeds United, Jack Harrison, mwenye umri wa miaka 26 anasakwa na Leicester City. ***(Telegraph)***

**JACKSON KUPIMWA AFYA**

MSHAMBULIAJI wa Villarreal na Senegal, Nicolas Jackson, mwenye umri wa miaka 21 atafanyiwa vipimo vya afya huko Bournemouth leo kabla ya kukamilisha uhamisho wake euro milioni 23 (£20.3m). ***(Guardian)***

**SILVA, CHELSEA KUTETA**

CHELSEA imeanza mazungumzo na mlinzi wa Brazil, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 38, kuhusu mkataba mpya huku mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Athletic)***

**MCKENNIE KUTUA LEEDS**

MAZUNGUMZO yanaendelea kati ya Leeds United na Juventus kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia mwenye umri wa miaka 24, Weston McKennie. ***(Fabrizio Romano)***

**ARSENAL YAMTAKA MCKENNIE**

KLABU ya Arsenal pia inafuatilia kuhusu upatikanaji wa Weston McKennie kutoka Juventus ya Italia. ***(Gazzetto dello Sport)***

**FRESNEDA ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL wapo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili beki wa pembeni wa Real Valladolid raia wa Hispania, Ivan Fresneda mwenye umri wa miaka 18. ***(Football Insider)***

**NAVAS ATAKIWA FOREST**

KLABU ya Nottingham Forest ingependa kumsajili mlinda mlango wa Costa Rica, Keylor Navas kutoka Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 36. ***(Mail)***

**BENTLEY ANUKIA WOLVES**

GOLIKIPA wa Bristol City mwenye umri wa miaka 29, Daniel Bentley, anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya kabla ya kusajiliwa na Wolves. ***(Birmingham Live)***

## DONDOO ZA SOKA
### MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AIWEKA MTEGONI PSG

### ●●● Ni kutokana na uamuzi wake wa kutofikiria kusaini mkataba mpya wa kuendelea...

**PARIS,** Ufaransa

MWANDISHI wa habari, Gerard Romero wa Hispania ameripoti, Lionel Messi huenda asiongeze mkataba wake na Paris Saint-Germain.

**Nahodha huyo wa zamani wa Barcelona mwenye umri wa miaka 35, mkataba wake na PSG unamalizika mwishoni mwa msimu, hivyo kuibua uvumi raia huyo wa Argentina anaweza kurudi Camp Nou akiwa huru.**

Rais Joan Laporta hapo awali alizungumza juu ya uwezekano huo ingawa ametulia katika siku za hivi karibuni, haswa na hali ya matumizi ya kifedha ya klabu mbaya.

Zaidi ya hayo, iliripotiwa Messi na PSG tayari walikuwa wamefikia makubaliano kimsingi ya kuendeleza ushirikiano wao kwa angalau msimu mmoja zaidi.

Lakini, Romero sasa amefichua Messi anakaribia kutoongeza mkataba wake na mabingwa hao wa Ligue 1.

Mwanahabari huyo amesema hii haimaanishi mchezaji huyo aliyebeba Ballon d'Or mara saba atarejea Barcelona katika majira ya joto.

Lakini inaacha mlango wazi kwa uwezekano wa kurudi kwenye uwanja wake wa zamani.

Messi aliondoka Barca msimu wa joto wa 2021 baada ya klabu hiyo kushindwa kuongeza mkataba wake ulioisha kutokana na hali mbaya ya kifedha.

Laporta amesimama na uamuzi wake wa kutokubali kuongezwa kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina huku akisisitiza alikuwa na maslahi ya klabu wakati anapokea simu hiyo.

Mazungumzo ya kurejea yamekuwa yakiendelea kwa muda mrefu sasa, lakini mambo yalikuwa kimya kwa sababu ya ripoti za kuanzishwa upya na PSG.

Lakini Romero sasa anadai Messi hataki kuendelea kucheza pale Parc des Princes.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,069,8

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
ATLETICO MADRID
1 | 1.95
X | 3.45
2 | 3.66

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JOSHUA KUPANDA ULINGONI APRILI




**LONDON,** England

BONDIA Anthony Joshua atarejea ulingoni dhidi ya Jermaine Franklin ifikapo Aprili Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa O2 Arena.


Bingwa huyo wa zamani wa uzani wa juu anakumbuka nyuma kwenye kipigo dhidi ya Oleksandr Usyk na kushindwa katika mechi yao ya marudiano ya Agosti baada ya kupoteza mataji kwa Mukraine huyo ambaye hajashindwa mnamo Septemba, 2021.

Kurejea kwake sasa kunakuja huku Franklin akitarajiwa mtihani wake wa kwanza chini ya kocha mpya Derrick James.

Franklin alisafiri kwenda jijini London Novemba, mwaka jana kumenyana na Dillian Whyte.

Franklin amewahi kushinda mapambano yake yote 21 ya kulipwa, akiwaangusha wapinzani wake 14.

Atapambana na mpiganaji anayetamani kurejea katika njia za ushindi Joshua, ambaye sasa amepoteza mapambano matatu kati ya matano ya mwisho yaliyotokana na kushindwa kwake dhidi ya Andy Ruiz Jr mwaka 2019.



## Rashford alitakiwa kujitoa zaidi

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amemtaka, Marcus Rashford kujitoa zaidi kwa Manchester United, ambapo Mholanzi huyo analenga kuifanya iwe timu bora zaidi katika soka duniani.

Rashford amefunga mabao nane katika mechi nane zilizopita na ndiye mfungaji bora wa United msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England ana wastani wa kufunga bao kila baada ya dakika 124, akiwa amefunga mabao 17 katika mechi 28 kutoka kwa mabao 12.8 yanayotarajiwa.

Mkataba wa Rashford unamalizika ifikapo mwaka 2024, lakini Ten Hag ana imani ataongezewa mkataba mpya.

"Hapa ndio mahali pazuri pa kuwa kwa sababu tunataka kuunda timu bora - kwanza England, kisha Ulaya, kisha ulimwenguni," alisema Ten Hag kabla ya mechi ya Jumatano ya nusu fainali ya Kombe la EFL dhidi ya Nottingham Forest.

"Ni siri, mazungumzo kati ya klabu na wachezaji, lakini anaelewa United ni klabu yake na pia katika mazingira haya, timu hii, anacheza soka lake bora zaidi.

"Anaweza kuleta sifa zake na timu hii inaweza kumsaidia katika nafasi nzuri ya kufunga mabao, timu inatengenezwa ili sifa zake zijitokeze.

## HABARI MICHEZO

861,169/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/01/23 | 18:00 | Hull City vs Queens Park Rangers | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 02. 28/01/23 | 18:00 | Blackburn Rovers vs Birmingham City | 2.27 | 3.20 | 3.15 |
| 03. 28/01/23 | 23:00 | Getafe CF vs Real Betis Seville | 2.95 | 2.95 | 2.55 |
| 04. 29/01/23 | 14:15 | FC Twente Enschede vs Feyenoord Rotterdam | 2.75 | 3.45 | 2.40 |
| 05. 29/01/23 | 15:00 | OGC Nice vs Lille OSC | 2.95 | 3.30 | 2.35 |
| 06. 29/01/23 | 15:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 07. 29/01/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Valencia CF | 3.10 | 3.25 | 2.28 |
| 08. 29/01/23 | 16:30 | Brighton & Hove Albion vs Liverpool FC | 2.65 | 3.50 | 2.45 |
| 09. 29/01/23 | 17:00 | AJ Auxerre vs Montpellier HSC | 2.45 | 3.30 | 2.80 |
| 10. 29/01/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs FC Nantes | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 11. 29/01/23 | 17:30 | Schalke 04 vs 1. FC Cologne | 2.95 | 3.40 | 2.29 |
| 12. 29/01/23 | 18:00 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 3.05 | 3.30 | 2.29 |
| 13. 29/01/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Atletico Madrid | 3.20 | 3.20 | 2.26 |
| 14. 29/01/23 | 18:45 | SC Cambuur vs Fortuna Sittard | 2.75 | 3.35 | 2.45 |
| 15. 29/01/23 | 19:30 | Bayer Leverkusen vs Borussia Dortmund | 2.46 | 3.50 | 2.65 |
| 16. 29/01/23 | 20:30 | RC Celta de Vigo vs Athletic Bilbao | 2.85 | 3.00 | 2.55 |
| 17. 29/01/23 | 21:00 | Boavista Porto vs Portimonense SC | 2.27 | 3.20 | 3.15 |


MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 26/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 10:45 | 5881 | Melbourne Victory vs Sydney FC | 2.55 | 3.25 | 2.67 |
| 11:00 | 4752 | Barito Putera vs Psis Semarang | 3.10 | 3.05 | 2.22 |
| 12:00 | 3772 | PSS Sleman vs Arema | 3.16 | 3.21 | 2.12 |
| 13:00 | 3750 | Keshla FK vs Sabayil | 2.55 | 3.11 | 2.59 |
| 14:00 | 1133 | Aizawl FC vs Mohammedan SC | 2.95 | 3.21 | 2.23 |
| 14:30 | 1466 | Esteghlal Tehran vs Malavan Bandar Anzali | 2.27 | 2.75 | 3.37 |
| 14:30 | 1612 | Persib Bandung vs Pusamania Borneo | 2.01 | 3.32 | 3.32 |
| 15:00 | 1447 | Egnatia Rrogozhine vs Kukesi | 1.97 | 3.01 | 3.84 |
| 15:00 | 3176 | Newells Old Boys vs CA Platense | 2.10 | 3.06 | 3.37 |
| 15:00 | 3510 | Gor Mahia vs FC Talanta | 1.59 | 3.51 | 5.37 |
| 15:00 | 4746 | CA River Plate (Arg) vs CA Central Cordoba SE Reserve | 1.76 | 3.37 | 4.25 |
| 16:10 | 5233 | Emirates Club vs AL Urooba | 1.65 | 3.63 | 4.57 |
| 16:15 | 1576 | Al-Hamriyah vs Masafi | 1.66 | 3.72 | 4.34 |
| 16:30 | 2482 | Al Nasr Salalah vs Sohar Club | 2.69 | 2.69 | 2.80 |
| 16:30 | 3118 | Nassaji Mazandaran vs Sepahan Esfahan | 3.57 | 2.95 | 2.08 |
| 17:00 | 4211 | FC Goa vs East Bengal | 1.40 | 4.46 | 6.22 |
| 18:00 | 2191 | Atlas U20 vs Santos Laguna U20 | 2.05 | 3.32 | 3.22 |
| 18:00 | 3025 | Sabah vs Neftchi Baku | 2.12 | 3.21 | 3.16 |
| 18:00 | 5701 | AL Faiha vs Al Hilal Riyadh | 9.55 | 5.19 | 1.25 |
| 18:00 | 5789 | Hassania Agadir vs FUS Rabat | 3.59 | 2.96 | 2.07 |
| 18:30 | 1116 | Lamia vs Apollon Paralimniou | 1.26 | 4.99 | 9.56 |
| 18:30 | 4416 | AL Musanaa vs Sur | 2.30 | 2.91 | 3.12 |
| 20:15 | 3353 | Sccm Chabab Mohammedia vs RS Berkane | 2.75 | 2.80 | 2.64 |
| 20:30 | 1301 | Panathinaikos vs PAOK | 2.28 | 3.10 | 2.95 |
| 20:30 | 5173 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.05 | 8.72 | 31.16 |
| 20:45 | 5471 | Groningen vs Cambuur | 2.22 | 3.22 | 3.13 |
| 21:00 | 1051 | Tennis Borussia Berlin vs Chemnitz | 5.58 | 4.45 | 1.44 |
| 21:00 | 2904 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs AS Tel Aviv University W | 1.79 | 4.15 | 3.32 |
| 21:00 | 3702 | Sevilla FC W vs SC Huelva W | 1.96 | 3.67 | 3.16 |
| 21:00 | 4399 | Al Ittihad Jeddah vs Al Nasr Riyadh | 3.89 | 3.42 | 1.82 |
| 21:30 | 2479 | SAO Bento SP vs Inter De Limeira SP | 2.46 | 2.86 | 2.91 |
| 21:30 | 4271 | Spvg Schonnebeck 1910 vs DJK Arminia Klosterhardt | 1.15 | 6.86 | 11.43 |
| 21:30 | 5443 | Hapoel Katamon Jerusalem W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 1.24 | 5.40 | 6.80 |
| 22:00 | 4152 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.07 | 2.64 |
| 22:30 | 4004 | Union Touarga vs Olympique Khouribga | 1.89 | 2.85 | 4.56 |
| 23:00 | 2217 | Tenerife Sur W vs Real Sociedad W | 3.31 | 3.62 | 1.92 |
| 23:00 | 2512 | Real Madrid vs Atletico Madrid | 1.95 | 3.45 | 3.66 |
| 23:00 | 3565 | Ajax vs FC Volendam | 1.11 | 8.68 | 14.80 |
| 23:15 | 5648 | Pacos Ferreira vs Benfica | 11.98 | 6.39 | 1.20 |
| 00:00 | 5967 | Chico vs Alianza Petrolera | 1.95 | 3.01 | 3.94 |
| 01:00 | 1050 | Uruguay U20 vs Bolivia U20 | 1.34 | 4.45 | 7.87 |
| 01:30 | 1229 | Mirassol SP vs SAO Bernardo FC SP | 1.95 | 3.10 | 3.77 |
| 01:30 | 4259 | Botafogo RJ vs Madureira RJ | 1.44 | 3.93 | 6.63 |
| 02:10 | 1766 | Deportes Tolima vs America De Cali | 2.06 | 3.06 | 3.48 |
| 03:10 | 2533 | Fluminense vs Boavista RJ | 1.33 | 4.56 | 7.88 |
| 03:30 | 4550 | Sao Paulo vs Portuguesa SP | 1.37 | 4.08 | 7.85 |
| 04:00 | 1047 | Zacatepec vs Venados FC | 1.77 | 3.48 | 4.05 |
| 04:00 | 5690 | AD San Carlos vs CS Herediano | 3.11 | 3.21 | 2.14 |
| 04:20 | 3286 | Atletico Nacional vs Once Caldas | 1.64 | 3.47 | 4.97 |
| 06:05 | 4493 | Club Atlas vs Santos Laguna | 2.41 | 3.29 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# ALIYEPIGA HAT-TRICK YA TANO LIGI KUU AANZA MAJIGAMBO

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA, Ibrahim Mkoko (pichani) wa Namungo FC ambaye juzi alifunga mabao matatu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam amesema siri ya kufanya vyema katika mchezo huo ni kusikiliza aliyomweleza kocha wake.

**Mkoko amefunga hat-trick ya tano katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ambayo bado inaendelea.**

Mabao hayo ya Mkoko yaliibeba Namungo iliyokuwa ugenini kupata ushindi wa magoli 3-1, akifunga dakika ya 41, 56 na dakika ya nne ya nyongeza kabla ya mchezo huo kumalizika.

"Mafanikio haya ya leo (juzi), niliyoyapata ya kupiga 'hat-trick' ni kufuata maelekezo ya mwalimu wangu na mimi mwenyewe kupambana. Nadhani baada ya kufanya hivi sasa imenipa tamaa na chachu ya kuendelea kufunga mabao kila mechi inayokuja," alisema mchezaji huyo mara baada ya mechi hiyo na kukabidhiwa mpira wake.

Hiyo ni 'hat-trick' ya tano kwenye Ligi Kuu msimu huu, ambapo mchezaji wa kwanza kufanya hivyo alikuwa ni straika wa Yanga, Fiston Mayele, ambaye aliipata Novemba 17, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, mechi dhidi ya Singida Big Stars, wakishinda mabao 4-1.

Nahodha wa Simba, John Bocco akiwa na rekodi ya kufunga 'hat-trick' mbili mpaka sasa kwenye ligi hiyo alifanya hivyo Novemba 19, mwaka jana, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, timu yake ikishinda mabao 4-0 dhidi ya Ruvu Shooting na Desemba 30, mwaka jana alipiga nyingine Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ilipoivurumisha Prisons magoli 7-1.

Ni siku hiyo na mechi hiyo hiyo, mchezaji mwingine wa Simba, Saido Ntibazonkiza, alipopiga 'hat-trick', hivyo takwimu kuonyesha zipo tano mpaka sasa.

## Simba kamili kuikabili Coastal Union

INATOKA UKURASA 24

walikuwa na kadi za njano adhabu imeisha na wanaruhusiwa kucheza mechi hiyo, lakini hata wale majeruhi (Mosses Phiri na Peter Banda), nao wanaendelea na mazoezi na wenzao," alisema Ahmed.

Azam FC itawakaribisha Dodoma Jiji kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

"Hii ni nafasi nyingine kwetu kutafuta heshima, tunaendelea kurekebisha mapungufu tuliyoyabaini kwenye kikosi chetu ili tuingie katika mechi hiyo tukiwa imara," alisema Hasheem Ibwe, Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC.

Ibwe alisema wanahitaji kujifuta 'machozi' baada ya kutokuwa na matokeo mazuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaelekea hatua ya lala salama.

Singida Big Stars yenye matokeo mazuri katika siku ya hivi karibuni keshokutwa itaikaribisha Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa CCM Liti, mkoani Singida wakati Namungo itakuwa mwenyeji wa Ihefu kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi.

Yanga ilitwaa taji hilo baada ya kuwafunga Coastal Union katika fainali zilizochezwa Julai 2, mwaka jana.




## Nabi: Nguvu zote kuongeza mabao

INATOKA UKURASA 24

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, Said Soud, aliliambia gazeti hili jana bado hajapewa taarifa yoyote kutoka TFF endapo barua hiyo itamfikia, watakutana na kuifanyia kazi haraka.

Soud alisema kamati yake itaendelea kufanya kazi kwa weledi na kila upande utafahamu ukweli.

"Hiyo barua kama ipo TFF basi itatufikia na kamati tutakutana na kuifanyia kazi , sitaweza kusema lini kwa sababu hadi sasa sijapata taarifa rasmi ya barua hiyo ya review ya shauri la nyota huyo," alisema Soud.

Kwa sasa Fei Toto anaendelea kufanya mazoezi binafsi ili kulinda kiwango chake wakati asubiri hatima ya shauri ambalo liliwasilishwa na Yanga.

# Michezo

Alhamisi Januari 26, 2023

Nipashe




Messi aiweka mtegoni PSG

UKURASA 21

# Kocha Nabi: Nguvu zote kuongeza mabao

## ●●● Atangaza rasmi kubadilisha mfumo huku akimtaja Fei Toto...

**Na Saada Akida**

WAKATI kesi ya kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' ikisubiri kupangiwa siku nyingine ya kusikilizwa, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema analazimika kubadilisha mfumo ndani ya kikosi chake kinachotarajia kuanza mechi za hatua ya makundi kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika kutokana na kukosekana kwa nyota huyo.

**Fei Toto ameendelea kushikilia msimamo wa kuondoka ndani ya kikosi cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, na tayari amewasilisha maombi ya kusikilizwa upya kwa shauri lake.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kiungo huyo bado yuko katika mipango ya benchi la ufundi la Yanga lakini kwa sababu kwa sasa hayupo, analazimika kutengeneza mfumo mpya mpaka pale hatima yake itakapojulikana.

Nabi alisema kikosi chake kimerejea kambini kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya mchezo ujao wa Kombe la FA dhidi ya Rhino Rangers.

Kocha huyo alisema wataingia katika mechi hiyo wakiwa makini kwa sababu watatambulisha mfumo mpya ambao bado wachezaji wake wapya wanaendelea kuufahamu.

Alisema hali ya wachezaji wake iko vizuri ikiwamo Kennedy Musonda ambaye alipata shida katika mechi iliyopita walipokutana na Ruvu Shooting na anamjumuisha kwenye mipango ya kuwakabili Rhino Rangers.

"Ni wiki ya maandalizi makubwa kwa sababu ya ratiba iliyoko mbele yetu, kila mmoja ndani ya timu anatakiwa kuwa makini, kutopoteza mechi hasa tunaenda kutetea mataji yetu (Ligi Kuu na Kombe la FA), tunahitaji kufikia malengo yetu, tunaendelea kujiandaa na mfumo mpya ambao muunganiko wake unahusisha wachezaji wapya na waliokuwapo tangu mwanzo wa msimu," Nabi alisema.

Alimtaja nyota wake mwingine aliyerejea kwenye kikosi ni Mganda Khalid Aucho na anatarajia atatoa mchango wake watakapoivaa Rhino Rangers.

"Tuna mechi na ratiba ngumu kwa sasa na tunahitaji kupata matokeo mazuri katika kila mchezo, tunaendelea kujiimarisha na kuwajenga wachezaji wangu kukaa tayari kwa mapambano," Nabi alisema.

Wakati huo huo, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesema limepokea barua kutoka kwa Fei Toto akiomba Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji kufanya marejeo ya kesi iliyofikishwa katika kamati hiyo inayomhusu.

Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema Fei Toto amewasilisha maombi hayo kupitia kwa mwanasheria wake kutokana na kutoridhika na uamuzi uliotolewa awali.

"Ni kweli tumepokea barua ya kuomba 'review' ya shauri lake, inafanyiwa kazi na inaangalia siku ya kusikilizwa, wadau wanatakiwa kuwa na subira, hilo lipo katika kamati na itafanya kazi yake," alisema Ndimbo.

INAENDELEA UKURASA 23



Beki wa Simba, Henock Inonga, aliyekuwa majeruhi sasa amerejea katika mazoezi ya timu hiyo ili kujiandaa na mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Coastal Union itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba kamili kuikabili Coastal

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuendelea kupata matokeo chanya katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara, kikosi cha Simba kimeanza kujiimarisha kuelekea mchezo wa hatua ya 32 bora ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Coastal Union utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wakati Simba ikiwa imeanza mazoezi Jumatatu kujiandaa na mechi dhidi ya Coastal Union, mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Yanga yenyewe inaendelea na mazoezi ya kuikaribisha Rhino Rangers kutoka Tabora, mechi itachezwa Jumapili.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili kikosi chake kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwakabili Coastal Union kwa sababu wanajua mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani.

Ahmed alisema hakuna mechi rahisi kwenye michuano hiyo kwa sababu ya aina ya mfumo wa mashindano hayo.

Alisema kikosi chao kinakamilisha programu zote muhimu chini ya makocha Juma Mgunda na Ouanane Sellami na wanaamini watapata matokeo mazuri na hatimaye kusonga mbele.

"Ndiyo maana Simba imekuwa na makocha wengi kwa sababu asipokuwapo Roberto Oliveira, basi Mgunda na Sellami wataendelea, tunakwenda kucheza mechi ya Kombe la FA, tunashukuru wale wachezaji wetu ambao

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >